# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatatu Machi 4, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581605

www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

0745 700710
LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital


**'Niliuza** gari ili nipate fedha za uteuzi kuwania kiti cha udiwani'

UKURASA 3

**Shirika** lashtuka vifo vitokanavyo na uzazi, latoa vifaa kuvikabili

UKURASA 18



**Mvua** ya mawe ilivyoangusha nyumba 70 na kuua kuku 300

UKURASA 18




**PULISIC ATISHIWA KIFO**

UKURASA 22



# Siri machozi ya Mzee Rukhsa hii

• **Ni** alipolia kwa mara ya kwanza mbele ya wanawe, wosia wake kwa familia hadharani; Samia: Profesa Janabi asipuuzwe... *Endelea ukurasa 2&17*



## Mfungwa adaiwa kunajisi mtoto nje ya gereza

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akisoma Quran wakati wa dua maalum (khitma) aliyoiandaa kwa ajili ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi kwenye viwanja vya maonesho Nyamazi, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**



**Bob Wangwe**
"Kumbana mtoa huduma kwa kumlazimisha kutoa huduma bora kwa gharama isiyolingana na huduma hiyo, maana yake ni kwamba ama mwananchi atalazimika kutoa fedha nyingine au atapewa huduma mbovu."



**Dk. Elizabeth Sanga**
"Afya si haki ya msingi tena kwa kila mwananchi. Si jambo la utu, ni biashara! Jambo hili ni hatari, hasa kwa wagonjwa wenye bima ya NHIF wanaopata huduma kwenye hospitali hizo."



**Godlisten Malisa**
"Serikali ilipie gharama za uendeshaji NHIF ili fedha zinazotolewa na wanachama zitumike katika tiba pekee na si vinginevyo."

KITITA KIPYA NHIF

# Huduma zarejea hospitali binafsi, wadau waibuka na hoja maalum

UK. 3

**MICHEZO** GAMONDI AMTAKA YEYOTE ROBO FAINALI UK.24 **KABWELA** UK.7

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza wakati wa dua maalum (khitma) ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi, kwenye viwanja vya maonyesho Nyamazi Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Siri machozi ya Mzee Rukhsa kwa Rais Samia yawekwa wazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KABLA ya kuanza kuugua miaka miwili iliyopita, Rais mstaafu wa awamu ya pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi alikuwa hajawahi kulia, mtoto wake, Abdullah Mwinyi alisema juzi.

Abdullah ambaye ni Msemaji wa Familia ya Mzee Mwinyi katika msiba huo wa kitaifa wa kifo cha Mzee Mwinyi, pia aliwaambia waombolezaji kwenye Uwanja wa Amani, Unguja juzi kwamba baba yao hakuwahi kuugua kabla ya miaka miwili iliyopita alipoanza kusumbuliwa na saratani ya mapafu iliyosababisha kifo chake.

Jana, Rais Samia Suluhu Hassan aliongoza wananchi katika dua maalum (hitma) ya kumwombea Mzee Mwinyi katika Viwanja vya Nyamanzi, nje ya Mji wa Zanzibar, huku Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi akiweka wazi kilichomliza baba yao baada ya kumwona Rais Samia aliyemtembelea kipindi anaumwa.

Baada ya dua hiyo, Rais Dk. Mwinyi alitoa siri ya Mzee Mwinyi kulia alipotembelewa na Rais Samia akiwa nyumbani kwake Mikocheni, Dar es Salaam.

Dk. Mwinyi alisema baba yao alilia kwa furaha kutokana na mchango mkubwa aliotoa Rais Samia katika kumhudumia kupata matibabu ndani na nje ya nchi.

**NASAHA ZA JANABI**

Katika hatua nyingine, Rais Samia ameahidi kuyaenzi maisha ya Mzee Rukhsa kupitia mambo makuu matatu ambayo ni kusimamia kikamilifu ustawi wa wananchi kwa kushamilisha sekta binafsi, kusimamia haki na kuwa na subira na ustahimilivu.

Ni ahadi aliyoitoa juzi kwenye Uwanja wa Amani katika salamu zake wakati wa kuaga mwili wa Mzee Mwinyi.

Rais Samia alisema atamkumbuka Hayati Mzee Mwinyi kwa kuishi misingi bora ya maisha katika maisha yake yote, huku akitaka wananchi wafuate ushauri wa kitaalamu wanaopewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kuimarisha kinga ya mwili.

"Ninakumbuka tukiwa kwenye matembezi ya hisani katika kampeni ya 'Afya Yangu Mtaji Wangu', tuliongozwa na Mzee Mwinyi na mara zote alikuwa anaongoza halafu anakwenda ananisubiri ninamfuata, ikabidi aanze kunifuata mimi, lakini baada ya muda kanipita tena kuonesha alivyokuwa imara," alisema.

Hali hiyo, Rais Samia alisema ilisukuma waandishi wa habari kumwulizi Mzee Mwinyi siri ya kuishi miaka mingi akiwa imara, akiwajibu "ni mazoezi", lakini siri ya pili kwa vijana wa kiume aliwataka wamfuate pembeni awaelezee vyema.

Kauli hiyo ya Rais iliibua kicheko msibani, waombelezaji walitabasamu kwa sekunde chache kwenye Uwanja wa Amani kisha kuendelea kusikiliza salamu za Rais Samia.

Mkuu wa Nchi aliendelea kusema kuwa kupitia Hayati Mwinyi, lipo fundisho la kuwa na uwezekano wa kujifunza mambo ukubwani na kuyatilia maanani, akimwelezea alivyoendelea kuishi na misingi hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya mazoezi ya kutembea kilomita tano kila siku alipokuwa na umri wa miaka 50 na kutenga nusu saa kuendesha baiskeli jioni.

"Alifanya hivyo ili kuwatia ari wananchi kufanya mazoezi kwa kuwa ni njia ya kujiimarisha na kujilinda dhidi ya magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza kama vile kisukari na presha na ni matumaini yangu sote tutajifunza kitu kuhusu mazoezi kwa kuanza na kuwa na nidhamu. Ninadhani hapa Prof. Janabi naye anaendeleza wosia huo," alisema Rais Samia na kuibuka kicheko tena miongoni mwa waombolezaji.

***SOMA ZAIDI KUHUSU MAMBO YALIYOWEKWA WAZI JANA NA FAMILIA YA MZEE MWINYI UK. 17**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
04/03/2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano tarehe 06/03/2024** kampuni ya **AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka **Dar es Salaam** kuelekea **Tunduma** kupitia Mikumi.
   Gari hilo lenye namba za usajili: **IT 1250/ ITC 700**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - 22m**
   **Upana - 4.5m**
   **Kimo - 4.6**

3. Gari litasafirisha mzigo kuanzia saa **12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*


# Mfungwa adaiwa kunajisi mtoto akiwa nje ya gereza

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MFUNGWA wa Gereza la Kalilankulukulu, Wilaya ya Tanganyika anadaiwa kunajisi mtoto mwenye umri wa miaka 14 (jina limehifadhiwa).

Inadaiwa kuwa mtoto huo, mkazi wa Kijiji cha Kawanzige, wilayani Mpanda alitendwa ukatili huo wakati akitoa shambani na wenzake.

Tukio hilo lilitokea Februari 29, mwaka huu saa 11.00 jioni katika eneo linalopakana na mashamba ya gereza hilo ambalo ni maarufu kwa kilimo cha mpunga.

Kabla ya kufanya tukio hilo, indaiwa kuwa mfungwa huyo aliwatishia na kuwateka watoto waliokuwa na binti huyo na kuwaweka chini ya ulinzi na ndipo alipomchukua binti huyo na kumpeleka kwenye kichaka kisha kumfanyia ukatili huo.

Pia inadaiwa kuwa mfungwa huyo alitenda ukatili huo wakati akichunga ng'ombe katika eneo hilo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kawanzinge, Emmanuel Machela, alisema jana kuwa alipata taarifa siku ya tukio saa tatu usiku kuwa mtoto huyo amenajisiwa na mfungwa wa Gereza la Kalilankulukulu wakati akitoka kupanda mpunga.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo alipiga simu kwa Mkuu wa Gereza Msaidizi na kumweleza, pia baadhi ya wananchi wa kijiji chake walikwenda kwenye gereza hilo na kutoa taarifa, lakini aliwataka kurejea kijijini kwa kuwa hapakuwa na uthibitisho wa madai hayo.

Alisema mtoto huyo alipimwa kwenye Zahanati ya Gereza Kalilankulukulu na kubainika amenajisiwa, lakini alipewa dawa na kuruhusiwa.

Mtoto anayedaiwa kutendwa ukatili huo, alisema jana kuwa kabla ya kufanyiwa kitendo hicho, mfungwa huyo alimkamata na kumfunga kwa sweta aliokuwa nalo usoni na kisha alianza kumnajisi na hata alipopiga kelele hakupata msaada.

Alidai kuwa mfungwa huyo alipomaliza haja zake, alimwuliza kama ana fedha ili amwachie vinginevyo, angeendelea kumfanyia ukatili huo, naye akajibu kuwa alikuwa na Sh. 2,000, ambayo mfungwa huyo aliichukua.

Baba mazazi wa mtoto huyo (jina tunalo) alidai ni kawaida kwa binti yake kwenda kufanya vibarua kwenye "mbuga za mpunga" na huwa anaondoka asubuhi na kurejea jioni, lakini siku hiyo hakurudi mapema hadi saa tatu usiku. Waliingiwa na hofu hadi mwanawe aliporejea nyumbani akiwa na mwenyekiti wa kijiji na kuwaeleza kilichomsibu.

Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Mpanda, Dk. Limbu Mazoya alithibitisha kumpokea mtoto huyo na kumpatia matibabu baada ya vipimo kuthibitisha alinajisiwa.

Kaimu Mkuu wa Gereza la Kalilankulukulu analiyetambulika kwa jina moja la Bosco, alipoulizwa na Nipashe kuhusu tukio hilo, alidai hana mamlaka kuzungumzia suala hilo na kumtaka mwandishi kumtafuta Mkuu wa Gereza.

HABARI KITAIFA

# Huduma zarejeshwa hospitali binafsi

**Na Waandishi wetu**

WAKATI huduma zikirejeshwa katika hospitali na vituo vya watoa huduma binafsi nchini kwa wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), wadau wameitaka serikali kushughulikia mzizi wa tatizo.

Ili kuepusha mvutano kujitokeza tena, wadau hao wameodhoresha mambo 13 wanayoona yanapaswa kufanyia kazi, ikiwamo kusitisha matumizi ya kitita kipya cha NHIF na kurudi kwenye kitita cha zamani.

Wadau hao ni pamoja na Chama cha ACT-Wazalendo kilichoitaka serikali kumaliza mvutano huo ili huduma zirejee vizuri na kuepusha madhila kwa wananchi, huku Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA) likitaja serikali kuboresha huduma za afya.

Waziri Kivuli wa Afya wa ACT Wazalendo, Dk. Elizabeth Sanga, alipozungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, alisema serikali inapaswa kusitisha kitita kipya na kufuta Sheria ya Bima ya Afya kwa kile alichodai haiondoi tatizo la ugharamiaji, uhimilivu, haiokoi NHIF wala haitasaidia kutoa unafuu kwa wananchi.

"Serikali ichukue pendekezo letu la kufungamanisha Bima ya Afya na Hifadhi ya Jamii ambapo kila mwananchi atakuwa na bima ya afya na atachangia kulingana na uwezo wake na apewa huduma kulingana na mahitaji yake.

"Pia iboreshe na kuongeza huduma za afya ya msingi ya zahanati na vituo vya afya ili kuimarisha huduma za kuzuia magonjwa na kupunguza idadi ya watu kwenye hospitali za rufani.

"Afya si tena haki ya msingi ya kila mwananchi. Si jambo la utu, ni biashara! Jambo hili ni hatari, hasa kwa wagonjwa wenye bima ya NHIF wanaoendelea kupata huduma kwenye hospitali hizo, ni wazi mgogoro huu utawaathiri zaidi wananchi," alisema.

Waziri Kivuli huyo alisema chama chao kinaona mgogoro huo ni matokeo ya huduma za afya kugeuzwa bidhaa kutokana na kutungwa sheria mbovu ya bima ya afya.

Mkoani Dar es Salaam jana, viongozi wa JUKATA na Asasi ya Umoja wa Kizazi cha Kuhoji (UTG), walitoa mapendekezo 13 ikiwamo kufumua Bodi ya Wakurugenzi wa NHIF kwa kile wanachodai imeshindwa kusimamia mfuko huo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe alishauri serikali kutafuta suluhu itakayokubalika na pande zote mbili, yaani NHIF na watoa huduma, ili kutoumiza wananchi ambao ndiyo walengwa wakuu.

"Kumbana mtoa huduma kwa kumlazimisha kutoa huduma bora kwa gharama isiyolingana na huduma hiyo maana yake ni kwamba ama mwananchi atalazimika kutoa fedha nyingine au atapewa huduma mbovu," alisema Wangwe.

Mwenyekiti wa UTG, Godlisten Malisa, alisema haungi mkono kitita kipya cha NHIF kuendelea kutumika wakati mazungumzo yanaendelea.

Alisema kamati ya kupitia upya kitita cha huduma ihusishe wadau wote kwa usawa wakiwamo wataalamu kutoka wizarani, NHIF, hospitali za umma, hospitali binafsi na wanachama wa mfuko huo.

Pia aliitaka serikali ihakikishe fedha zilizokopwa NHIF zinarejeshwa, watumishi waliotajwa katika ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (CAG) kuhusika na ubadhirifu wa fedha katika mfuko huo wachukuliwe hatua na kulipwa kwa madeni yaliyotokana na huduma za bure kwa wazee.

"Serikali ihakikishe watumishi 146 waliotajwa katika ripoti ya CAG kuhusika na ubadhirifu wa Sh. bilioni 14 wanachukuliwa hatua ikiwamo kufikishwa mahakamani," alisema Malisa.

Mapendekezo mengine ni pamoja na serikali kulipia gharama za uendeshaji za mfuko huo ili fedha zinazotolewa na wanachama zitumike katika tiba pekee na serikali kulipa kwa wakati vituo vya kutolea huduma badala ya kulimbikiza madeni.

Kukiwa na hoja hizo, uongozi wa Hospitali ya Regency ya Upanga, jijini Dar es Salaam umekubali kuendelea kutoa huduma wakati mazungumzo yakiendelea.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya ujumbe wa NHIF, ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga kutembelea hospitali hiyo Jumamosi kuangalia namna huduma zinavyotolewa.

Konga aliomba radhi wanachama wa NHIF kwa usumbufu waliopata, akiwahakikishia wameshazungumza na uongozi wa hospitali na wamewahakikishia huduma zitaendelea kama kawaida.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa hospitali hiyo, Lalit Kanabar alisema waliandika barua kwa NHIF kuhusu utayari wao wa kuendelea kutoa huduma kwa wanachama wa NHIF.

"Tumekutana na uongozi wa NHIF tumezungumza na tumekubaliana huduma ziendelee wakati mambo mengine yanaendelea kujadiliwa na tumesha-saini mkataba na huduma kwa wanachama wa NHIF zimerejea," alisema Kanabar.

Mmoja wa wagonjwa waliokuwa hospitalini huko, Faraja John alishukuru NHIF kwa kutembelea baadhi ya hospitali kuangalia namna huduma zinavyotolewa.

"Tulipata mshtuko kusikia huduma zitasitishwa lakini baada ya kuwaona NHIF kuja hapa na kutuhakikishia huduma zipo, tunaona faraja kwamba sasa tutapata huduma bora kama mwanzo," alisema. NHIF ilitangaza kuanza kwa matumizi ya kitita kipya cha matibabu kuanzia Machi Mosi, mwaka huu, hali ambayo ilisababisha mvutano kati yake na chama cha watoa huduma binafsi za afya (APHFTA). Baadhi ya hospitali hizo zilizotangaza uamuzi wa kutowapa huduma wanachama wa NHIF, ni Aga Khan, Masana, Regency Medical Centre, TMJ, Kairuki na Boch, huku Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akiingia kati kwa kuzipa onyo.

***Imeandikwa na Joseph Mwendapole, Halfani Chusi na Maria Seme**

# 'Niliuza gari ili nipate fedha kuteuliwa kuwania udiwani'

**Na Salome Kitomari**

WANAWAKE waliowahi kushiriki Uchaguzi Mkuu na ule wa Serikali za Mitaa wameeleza madhila waliyopitia, huku wakitaka vyama kuharakisha maboresho ya sheria kujumuisha suala la jinsia.

Mmoja wao amedokeza kuwa alilazimika kuuza gari lake ili apate fedha za kumwezesha kuteuliwa kuwa mgombea udiwani, na hakuteuliwa.

Wakati wa kongamano la Siku ya Wanawake mwishoni mwa wiki lililoandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) jijini Dar es Salaam, wanawake hao walitaja madhila hayo yanajumuisha:

Kuombwa fedha, rushwa ya ngono, kudhalilishwa, kuambiwa nafasi hizo ni kwa ajili ya wanaume, kutoaminiwa na jamii husika pamoja na kuombwa rushwa ya fedha, vitu na ngono ilivyokithiri wakiitaja ni hali inayopunguza ushiriki wa wanawake kwenye siasa.

Aliyekuwa mtiania ya kugombea udiwani Kata ya Kitunda, Prisca Ngweshemi, alieleza madhila aliyopitia ikiwamo kuombwa rushwa ya fedha na ngono, kuzuiwa kwenda kwenye mikutano ya mitaa na jina kukatwa kwenye vikao vya juu kwa sababu hajatoa wanachokitaka wajumbe.

"Unapotangaza nia ya kugombea uwe na fedha, kanga, dhahabu, kama huna fedha uchaguzi ni mgumu sana. Mimi niliuza gari nililopewa zawadi na mume wangu, fedha ziliisha na sikuambulia kitu, unakutana na wajumbe wanakwambia 'una sifa zote ila wewe ni mchungu'.

"Unakuta unatakiwa utembelee mtaa fulani, lakini vijana wameweka vizuizi usiwafikie wajumbe wanakwambia kabisa tumelipwa kufanya hivi, ukitaka upite nawe tulipe kiasi hiki. Wengine wanakutamkia kabisa wanataka mwili wako.

"Nilipambana yalirudi majina mawili la mwanaume na langu, lakini baadaye sikushinda kwa sababu sikuwa na fedha za kugawa," alisema.

Mjumbe kutoka Mtaa wa Vijibweni, Vatherine Valence, alisema "Mwaka 2020, niligombea ila jina liliondolewa kwa kigezo sijui kusoma na kuandika.

"Fikiri Msomi na mkufunzi wa chuo kikuu ninaondolewa eti sijui kusoma na kuandika. Ndio maana tunasema uchaguzi wa serikali za mitaa usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na si Waziri wa TAMISEMI.

"Huu ni uchaguzi muhimu kwa sababu ndio wananchi waliko, ukiwa kiongozi ngazi hii unaishi na wananchi wa chini kabisa ni muhimu kufanya marekebisho," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa CHADEMA, Susan Lyimo, alisema mwaka 2020 chama hicho kiliweka wagombea 500 kwenye mitaa, lakini walikatwa wakabaki 22, jambo ambalo alisisitiza halikubaliki.

Akiwasilisha ripoti ya uchaguzi wa serikali za mitaa, Mtafiti Victoria Lihiru, alisema kati ya wenyeviti wa vijiji 11,669 nchini, wanawake ni 246 (asilimia 2.1), huku vitongoji ni 62,612 wanaume ni 58,441 na wanawake 4,171 huku kwenye mitaa 3,643 wanaume ni asilimia 67.4 na wanawake ni asilimia 12.6 pelee.

www.panafricanenergy.co.tz

Ni kwa masikitiko makubwa tunatoa salamu za pole kwa Serikali na watu wa Tanzania kufuatia msiba wa Rais wa Pili wa nchi yetu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. Tunaungana na taifa katika kuomboleza kifo cha kiongozi huyu mahiri aliyekuwa na nafasi kubwa katika historia ya Tanzania.

BURIANI

Mhe. Ali Hassan Mwinyi

Rais Mstaafu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

1925 - 2024



PANAFRICAN ENERGY an Orca Company



Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Edwin Masue, akimpima shinikizo la damu mkazi wa Dar es Salaam aliyefika katika kambi maalumu ya siku mbili inayoendeshwa na wataalamu wa afya wa hospitali hiyo katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JKCI**

DK. ASHA MAHITA:

# Miundombinu ya afya imeimarishwa, kikwazo ni matabibu kukosa uadilifu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeimarisha vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Watumishi waadilifu, wenye weledi na wanaojali wagonjwa ndiyo changamoto kwa sasa.

Ni kauli ya Mratibu wa Tiba ya Wagonjwa Wanaotibiwa Nje na Tiba Utalii - Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita aliyoitoa katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Alitaka watumishi na wataalamu wenzake wa afya kuwa waadilifu, wazingatie weledi na wasidai wala kupokea zawadi kutoka kwa wagonjwa ili kufanikisha azma ya serikali ya kutibu Watanzania wanapowahitaji.

Katika mazungumzo hayo yaliyoangazia pia mafanikio ya utumishi wake wa miaka 21 katika sekta ya afya, Dk. Asha aliwataka madaktari na wauguzi kutoa huduma kwa moyo na unyenyekevu bila kudai au kupokea chochote.

Kwa watumishi wa afya, wakiwamo madaktari chipukizi, Dk. Asha alitoa ushauri mahususi kwao, akisema "Kutibu ni wito, hivyo ni vyema kuwa na hofu ya Mungu unapotimiza majukumu yako.

"Sisi tunasimama hapa kwa niaba ya Mungu kuponya na kulinda uhai, Mungu ndiye mganga mkuu. Tufanye kazi kwa kujitoa na kuwa na upendo na kujali wagonjwa. Tuwe na ukarimu kwa wagonjwa wetu, ni muhimu mno.

"Madaktari, wauguzi na watumishi tuwe na lugha nzuri, tujisafishe, tuwahudumie wagonjwa kwa upendo. Tujue ugonjwa unatuhusu sote. Leo wewe, kesho shida inakuwa kwangu."

Akifafanua zaidi kuhusu angalizo lake kwa watoa huduma dhidi ya zawadi toka kwa wanaowapa huduma, Dk. Asha alisema wagonjwa wana tabia ya kushukuru madaktari na wauguzi, lakini si lazima mtoa huduma za afya apokee shukrani hiyo, iwe fedha au bidhaa.

"Ni muhimu tutoe huduma za afya, mwananchi au mteja ahudumiwe katika mazingira bora, kwa wakati, kwa utaalamu na weledi, huku mtoa huduma akitumia lugha nzuri na kumpa matumaini," alisema.

Dk. Asha alisisitiza matibabu wenzake wakatae zawadi ili watu na wagonjwa wafahamu kuwa kutibiwa ni haki yao wala hawalazimiki kuwapa vitu au fedha madaktari na wauguzi.

Alisema kuna changamoto katika utoaji huduma za afya nchini, lakini zitapungua kwa kujali zaidi na kuhudumia wateja ambao ni wagonjwa bila kupewa, kuomba au kupokea kitu ili kuwatibu.

Dk. Asha alisema kuwa zamani wakati anaanza kazi kwenye Hospitali ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru), sekta ya afya ilikuwa haijaimarika kama ilivyo leo. Mambo mengi ya zamani yalikuwa magumu.

Katika hilo, alitolea mfano kwamba katika zama zao, daktari wa zamu, alishika maeneo mengi na kuyasimamia; dharura, upasuaji na hata wodi ya wazazi, yote yalimngoja kutokana na uhaba wa watumishi.

"Leo sekta ya afya imepiga hatua sana. Kuna teknolojia ya kidijitali. Wapo mabingwa, vifaa na utaalamu wa kielektroniki kwenye maabara, vipimo na mawasiliano. Ni muhimu kuridhika na kuwajali wateja," alisema.

Mratibu huyo pia aliwataka madaktari na watumishi kujifunza uvumilivu, kufanya kazi kwa upendo na kuridhika kwa kuwa "huwezi kupewa kila kitu na hata ikitokea ukapewa huenda usiridhike".

Aliongeza: "Ni wito wangu ninapotimiza miaka 21 ya utumishi ndani ya sekta ya afya, tutoe huduma bora kwa mteja. Mgonjwa aridhike, hicho ndicho kikubwa kwake na kwetu pia."

Dk. Asha ambaye alikuwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Temeke, alisema kuwa mabomu yalipolipuka kwenye kambi ya jeshi Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam, aliwahimiza matabibu wenzake kutoa huduma kwa utu na kuwapa huduma bora wagonjwa, akisisitiza hali ilikuwa mbaya.

Alipongeza mikakati ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuimarisha miundombinu, utaalamu na vifaa tiba, akihimiza matatibu wenzake kuwajibika zaidi.

Dk. Asha, mtoto wa Mkuu wa Jeshi la Polisi mstaafu, IGP Omar Mahita, alihitimu masomo ya utabibu Ukraine. Mbali na Hospitali ya Temeke na Mount Meru, aliwahi kufanya kazi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala.

Vilevile, Dk. Asha (50), alikuwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Temeke na Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam. Kitaaluma ni daktari wa binadamu.

# 'Msinyanyapae wanaotoa harufu mbaya kinywani'

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Msaidizi Huduma za Kinywa na Meno katika Wizara ya Afya, ameitaka jamii kuacha kunyanyapaa watu wanaotoa harufu mbaya ya kinywa.

Badala yake, Dk. Baraka Nzobo, ameelekeza waambiwe ukweli kwa upole na upendo kuhusu tatizo walilonalo na kuwashauri kwenda hospitalini kuonana na daktari wa kinywa na meno.

Mkurugenzi huyo alielekeza hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusu afya ya kinywa na meno.

Alisema mdomo hutoa harufu kutokana na bakteria wanaotoa gesi inayofanana na gesi inayotoka kwenye yai lililooza la ndege kama kuku au bata.

"Mdomo kutoa harufu mbaya huchangiwa kwa asilimia 80 hadi 90 na bakteria waliopo maeneo ya kinywa, hasa kwenye utando wa ulimi, ndani ya jino lililooza na katika utando mgumu kati ya jino na fizi (ugaga).

"Bahati mbaya Watanzania wengi wenye tatizo la kunuka mdomo, hawatambui kama midomo yao inanuka, mpaka waambiwe na mtu wa karibu, tena wenye upendo na wanaojiamini.

"Ni ngumu sana kumwambia mtu kuwa 'mdomo wako unatoa harufu mbaya', zaidi utakuwa unamkwepa pale unapokutana naye.

"Tatizo hili la kutoa harufu mbaya mdomoni linasumbuwa watu wengi, kuanzia wasomi, wasio wasomi, matajiri na maskini," alisema Dk. Nzobo.

Alisema tatizo hilo linasumbua watu wa maeneo yote bila kujali ni mijini au vijijini, kwa kuwa tatizo la kuoza meno nchini lipo kwa asilimia 76.5 ya watu wazima na asilimia 31.1 ya watoto.

"Mdomo kuwa na harufu kama yai lililooza, asilimia 10 hadi 20 huchangiwa na sababu zilizo nje ya kinywa cha mwanadamu. Kama vile lishe duni, magonjwa ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula, uvutaji sigara, mafua sugu na matatizo mengineyo," alisema Dk. Nzobo.

Alitaja dalili za magonjwa ya fizi ni pamoja na fizi kuvimba, fizi kutoa damu kiurahisi, kutema damu wakati wa kupiga mswaki, harufu mbaya mdomoni isiyoisha, meno kulegea na maumivu kwenye fizi inapoguswa na kitu chochote.

"Dalili za jino lililotoboka au kuoza ni maumivu mfululizo ya jino, maumivu makali ya jino usiku wakati umelala, jino kufa ganzi au kuuma wakati wa kula au kunywa kinywaji cha moto au baridi, mdomo kutoa harufu mbaya na jipu dogo kwenye fizi.

"Athari za kunuka mdomo zipo za aina mbalimbali kwenye jamii zinazokumba watu wenye midomo inayonuka; kusemwa mtaani au ofisini kuwa unanuka mdomo bila wewe kusikia.

"Baadhi ya marafiki watakukwepa kufanya nao mazungumzo kwa kuwa tu mdomo wako unanuka. Kuvunjika uhusiano wa kimapenzi -- watu wachache sana wanaweza kuendelea na uhusiano wa kimapenzi na wenzi wanaotoa harufu mbaya mdomoni," alisema.

Daktari huyo alisema athari zingine za tatizo hilo ni mtu anayefahamu kuwa mdomo wake unatoa harufu mbaya, hujinyanyapaa mwenyewe na kuanza kujitenga kukaa kwenye mikusanyiko kuongea na watu au kukutana na watu.

"Watu hugeuza au kukwepesha sura zao wanapoongea na mtu anayetoa harufu mbaya mdomoni. Jambo hili humwathiri kisaikolojia mlengwa anayenuka mdomo," alifafanua.

Alitoa rai kwa jamii kwenda hospitalini kufanyiwa uchunguzi wa vinywa vyao kupatiwa matibabu sahihi ya kusafishwa vinywa vyao, iwapo wana magonjwa ya fizi na pia watazibwa meno yao yaliyooza au kutoboka.

Dk. Nzobo pia alisema iwapo jino limeharibika vibaya, litang'olewa. Matibabu sahihi husaidia kuondokana na tatizo la kunuka mdomo.

"Watanzania wajenge tabia ya kupiga mswaki meno yao kwa dawa ya meno yenye madini ya floridi asubuhi na usiku, kabla ya kwenda kulala. Watu wengi hupiga mswaki asubuhi tu na kusahau kupiga mswaki usiku wanapokwenda kulala.

"Wazazi wawasimamie na kuhakikisha watoto wao wanapiga mswaki meno yao asubuhi na usiku wanapokwenda kulala, kumbuka pia kusafisha ulimi ili kuondoa utando wenye bakteria wanaoleta harufu mbaya mdomoni.

"Tusione aibu kuwauliza watu wetu wa karibu watuambie ukweli kama midomo yetu inanuka au hainuki," alishauri mtaalamu huyo.

## TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga zikiepuka haya, nusu fainali CAF inawezekana

**KLABU** kongwe za Simba na Yanga zimeiheshimisha nchi kwa kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mara ya kwanza tangu nchi ipate Uhuru mwaka 1961, timu mbili za Tanzania zimekwenda robo fainali kwa pamoja, ikiwa ni moja kati ya mafanikio makubwa katika soka nchi.

Ni Tanzania pekee iliyopeleka timu mbili kwenye hatua hiyo huku zilizobaki, zikiwamo zile kubwa kwenye historia ya soka barani Afrika zikipeleka timu moja moja tu.

Hii ni heshima kubwa ya soka la Tanzania ambalo linaonekana limekuwa likipanda siku moja baada ya nyingine kuelekea kwenye mafanikio yanayotarajiwa na viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), serikali na Watanzania kwa ujumla.

Kwa hili tusiache kuwapongeza wote wanaohusika kuanzia wawekezaji ambao pamoja na kwamba michakato ya mabadiliko kwenye Klabu za Tanzania hasa hizi kubwa imekuwa ikifanywa kwa mwendo wa kinyonga, lakini hawakati tamaa, badala yake wamekuwa bega kwa bega na klabu katika kuzihudumia kambi, chakula, safari, malazi, posho, mishahara na usajili wa wachezaji bora ambao ndio wamezifanya kufika hapa.

Wangeweza kukaa pembeni hadi mabadiliko yatakapokamilika, lakini kwa mapenzi yao wenyewe kwa klabu hizo, pamoja na kujali furaha za watu wengine, wameamua kubeba mizigo ya gharama bila kujali, wakati mwingine wakibezwa na kutukanwa na baadhi ya watu.

Hapa tunawazungumzia Mohamed 'Mo' Dewji wa Simba na Ghalib Mohamed wa Yanga hawa wamekuwa nyuma ya furaha ya Watanzania ambao wakati mwingine hawana maisha mazuri wala kipato, lakini wamekuwa na furaha tu kwa sababu timu zao zinashinda.

Hata hivyo, pamoja na dhamira yao ya dhati kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu ambao si wema kutaka kuzihujumu timu hizi, hasa kwenye mechi za kimataifa ili zifungwe.

Kumekuwa na taarifa nyingi tofauti kuwa baadhi ya watu wa upande mmoja wanasaidia upande mwingine ili watoke kwenye mashindano. Hili huwezi kulipa jina lolote zaidi ya hujuma chafu. Na haina tofauti yoyote na kuhujumu nchi.

Timu ya Tanzania inajiandaa kucheza mechi ya kimataifa, halafu mashabiki au viongozi wa timu nyingine wanahusishwa na kuwasaidia wageni ni hujuma tu kama zingine zozote.

Katika soka haikatazwi shabiki wa Simba kwenda kuwashangilia wapinzani wa Yanga, au wa Yanga kwenda kuwazomea Simba wakicheza na wageni, lakini si kufanya hujuma yoyote ile ya nyuma ya pazia na iko kinyume na mambo ya michezo ili ifungwe.

Hivyo, rai yetu ni kutaka kuona baada ya Simba na Yanga kutinga hatua hii, tunaiomba serikali ikae macho na watu wenye tabia hiyo kwa manufaa ya nchi kwani hata salamu za pongezi za Rais wa Jamburi ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwa timu hizo ziliposhinda, alisema hiyo si furaha yao pekee bali ni kwa Watanzania wote kwa ujumla.

Hutuwezi kujua, inawezekana zote zinapita kwenda nusu, au kukutana fainali, hivyo serikali kuanzia wizara yenyewe inayohusika na michezo, Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), na hata Usalama wa Taifa, waanze kuwa makini na watu waliokuwamo kwenye klabu hizo kutaka kuhujumiana.

Mafanikio ya timu hizo ni mafanikio ya nchi kwa ujumla na kama ni figisu basi ziishie humu humu kwenye mechi za Ligi Kuu, lakini si kwa timu inayobeba bendera ya nchi.

Mtu yeyote ambaye nchi iko vitani halafu yeye anazuia ama anauza mbinu za askari wa taifa lake ili wapigwe, huyo ni adui namba moja na anapaswa kushughulikiwa ipasavyo kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Majaji lindeni mchezo wa ngumi, si kuwabeba mabondia

Na Adam Fungamwango

**UKIPITA** mitaani utakuta kila mmoja akiwa hakubaliani na sare aliyoipata bondia Mtanzania, Selemani Kidunda.

Hata watoto nao ukiwauliza wanakwambia, bondia Mtanzania alikuwa amepoteza pambano na hawaelewi kwa nini imekuwa sare.

Watanzania pamoja na uzalendo wao wote, lakini hili wameonekana kutokubaliana nalo, na inaonekana kama unaongea na raia wa Afrika Kusini.

Nilimsikia mama mmoja mtu mzima akisema anajuta kwa nini amepoteza usingizi wake.

"Bora ningelala kuliko hiki nilichokiona. Mimi ni Mtanzania na nilipenda bondia wetu ashinde, lakini kwa hiki nilichoshuhudia, bondia wetu amepoteza pambano, na wala si sare, imeniuma sana, mtoto wa watu wamemnyima ushindi," alisikika akisema bibi huyo akiwaambia wajukuu zake.

Kila unapopita asubuhi ile ya Machi 2, utasikia watu wanalalamikia juu ya maamuzi ya pambano lililopigwa usiku wa Machi Mosi, mwaka huu, Masaki jijini Dar es Salaam kati yake dhidi ya Asemahle Wellem kutoka Afrika Kusini.

Lilikuwa ni pambano la uzito wa Super Walter lililokuwa na raundi 12 ambazo ziliisha zote.

Kilichotokea hapo ni kwamba Watanzania hawakuridhika na maamuzi. Licha ya watu kulalamika kila unapokata kona, kwenye mitandao ya kijamii ndiyo kabisa.

Ukisoma maoni ya watu utaona kabisa kuwa kuna kitu hakiko sawa kwenye pambano hilo na itabidi sasa majaji wabadilishe mitazamo yao.

Ni kweli ndondi ina ufundi wake katika upiganaji, ambapo kuna maeneo yana pointi nyingi kuliko zingine, unaweza kuona bondia kapiga ngumu nyingi, lakini hazina alama nyingi, lakini chache zikipigwa mwingine akipiga chache zenye alama nyingi, lakini kuna vitu vingine vinaonekana kwa macho, tena na watu wengi.

Kama ilikuwa ni kupiga kura kwa watazamaji na si pointi za majaji, bondia Wellem angeibuka na ushindi kutokana na umahiri wake aliokuwa akiuonyesha ulingoni na jinsi alivyokuwa akitawala, pia staili yake ya upiganaji na jinsi alivyokuwa akirusha ngumi zake kwa ufundi mkubwa.

Na wala haikushangaza kuona mwisho wa pambano hilo, Kidunda akiwa amechakaa uso, huku mwenzake akiwa kama ametoka disko.

Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema kama Kidunda ndiyo angekuwa Wellem, basi ushindi ungeenda kwake.

Angalau malalamiko mitaani na kwenye mitandao ya kijamii yalipunguzwa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Simba dhidi ya Jwaneng Galaxy, ambapo Watanzania na mashabiki wa michezo waligeukia huko na kuachana na matokeo ya ndondi ambayo yamepigwa na Watanzania wengi.

Kinachoonyesha huenda Watanzania wakawa wako karibu na ukweli, ni kwamba walikuwa nyuma na kuumuunga mkono bondia wao kwa namna ya uzalendo, lakini sare hiyo hawakukubaliana nayo.

Niliona hivi karibuni baadhi ya mashabiki wakipinga ushindi na baadhi ya mabondia wa Kitanzania wanapigana na mabondia kutoka nje hapa nchini.

Na kwa siku zinavyoendelea inaonekana wanakosa imani nao, wengine wakienda mbali zaidi wakitaka majaji kutoka nje ya nchi ndiyo wafanye kazi hiyo.

Binafsi, naona kama hicho ni kengele cha hatari kwa mchezo wa ngumi ambao kwa sasa unashika nafasi ya pili kwa umaarufu na kupendwa nchini.

Kutokana na kurejea kwa wadhamini na kuanza kuonyeshwa kwenye televisheni, mchezo wa ngumi umerudi kwenye chati kama ilivyokuwa zamani, hivyo kinachotakiwa si kuwalinda mabondia wa Tanzania, lakini si kuwasaidia kushinda.

Kwa sasa unaangalia na kufuatiliwa na watu wa rika zote, wengine wanakesha, sasa kama wameanza kuguna na unaanza kukosa mvuto na anayeshinda hapewi haki yake, wataanza kuudharau na kuendelea kufuatilia vitu vingine.

Kama hata kinamama wanaacha tamthilia na kufuatilia ngumi, halafu mwisho wa siku maamuzi hakubaliani nayo, kesho yake hawatofuatilia tena.

Kama mchezo huu utapoteza tena mashabiki basi ni majaji watakuwa wamefanya hivyo. Binafsi naomba waendelee kuulinda mchezo kwa kutoa maamuzi ya haki ili uendelee kupendwa na si kuwafurahisha wachache kwa kuwapa kisichostahili mabondia wa Tanzania.

Tuwaache washinde kwa uwezo wao na nina uhakika wanapopigwa ndipo wanakwenda kujipanga ili kushinda pambano lijalo. Wanapopata ushindi au sare isiyoeleweka wanabweteka.

HABARI KITAIFA

# Atupwa gerezani miaka 30 kwa kunajisi mdogo wake

**Na Joctan Ngelly,** MISSENYI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Missenyi Mkoa wa Kagera imemhukumu Marius Steven (19), mkazi wa Bunazi kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kunajisi mdogo wake.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Jane Byemelwa baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Byemelwa alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama hizo.

Alisema Upande wa Mashtaka, ukiongozwa na Inspekta wa Polisi Zakayo Napegwa, ulipeleka mahakamani huko mashahidi watano na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Byemelwa alisema kuwa siku ya tukio hilo, Novemba 18, 2023, saa saba usiku, katika Kijiji cha Bunazi, Wilaya ya Missenyi, mkoani Kagera, mshtakiwa aliingia kwenye chumba cha mdogo wake (wa tumbo moja) ambaye ni msichana mwenye umri wa miaka 17 na kumkuta amelala, alimshika kwa nguvu na kumvua nguo kisha kumnajisi.

Alisema kuwa baada ya mshtakiwa huyo kunajisi mdogo wake, binti huyo alipiga kelele ndipo wazazi wao pamoja na majirani walifika eneo la tukio hilo na kukamata mshtakiwa huyo na kumpeleke Kituo cha Polisi Kyaka na alipohojiwa alikiri kuhusika na kosa hilo.

Hakimu alisema mwathirika wa tukio hilo alipewa Fomu Namba Tatu ya Polisi (PF3) na kupelekwa Kituo cha Afya Bunazi, alikofanyiwa uchunguzi na daktari na kuthibitishwa kuwa kweli alinajisiwa.

Alisema kuwa baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika, mshtakiwa alifikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Hakimu Byemelwa alisema amesikiza ushahidi wa pande zote na kubaini kuwa Upande wa Mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama inamtia hatiani mshtakiwa.


Mwendesha Mashtaka Inspekta wa Polisi, Zakayo Napengwa alidai mahakamani huko kutokuwa na kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa.

Alidai kitendo alichokifanya mshtakiwa ni cha kikatili na kinadhalilisha jamii, hivyo akaomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama yake.

Mshtakiwa huyo wakati wa kuomba kupunguziwa adhabu, alidai ni kosa lake la kwanza, hivyo akaomba mahakama impunguzie adhabu kwa sababu ana familia inayomtegemea.

Hakimu Byemelwa alisema kitendo alichokifanya mshtakiwa hakikubaliki, ni cha aibu katika jamii, hivyo mahakama inakuhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani ili iwe ni fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama zake.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Inspekta wa Polisi Zakayo Napegwa alidai kuwa Novemba 18, 2023, saa saba mchana, kijijini Bunazi, wilayani Missenyi, mshtakiwa alinajisi mdogo wake ambaye ni msichana mwenye umri wa miaka 17 na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri. Kitendo hicho ni kinyume cha sheria.




Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Security, Eric Sambu (wa pili kushoto), akionyesha Tuzo ya Huduma Bora ambayo kampuni hiyo ilipokea jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine kutoka kushoto ni Elizabeth Muzo kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mkurugenzi wa Biashara za Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi John Ulanga na Mkurugenzi Mkuu wa CICM Global ya Zimbabwe, Rinos Mautsa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kaya 900 zamlilia Rais mgogoro na mwekezaji

**Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya kaya 900 za kijiji cha Lupunga, Kibaha mkoani Pwani, ziko hatarini kukumbwa na njaa baada ya kinachodaiwa na mwekezaji kuvamia mashamba na kuharibu mazao kinyume cha sheria.

Kutokana na mgogoro huo, kaya hizo zimemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia kabla ya kukumbwa na majanga.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Mwenyekiti wa Kitongoji, Abdalah Selemani, alisema mgogoro wao na mwekezaji aitwaye Continental ni wa muda mrefu na amedai kuwa amekuwa akikingiwa kifua na uongozi wa mkoa. Alisema mwekezaji huyo mara ya kwanza alikwenda kwenye kijiji na kudai ni chake jambo ambalo uongozi haukumwelewa na kuhitaji uthibitisho eneo hilo amelipataje.

"Ilipofika hatua hiyo, hakuwa na uthibitisho. Alikwenda katika uongozi wa mkoa kuomba msaada na mpaka kufikia hatua ya kupata jeuri ya kuharibu mazao na mali za wananchi," alisema.

"Kiukweli wananchi wanaumia sana na kadhia hii wamechoka. Tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan atusaidie kupata haki yetu kwa sababu mkoa umeshindwa kufikia mwafaka naye," alisema.

Alisema kuwa kilio chao walimpelekea waziri mwenye dhamana ambaye aliwapa ahadi kwamba atalishughulikia lakini kabla ya majibu yake, mwekezaji alivamia maeneo ya wananchi na kuharibu mazao mbalimbali.

"Ninakumbuka siku ya tukio lilikuja buldoza kwenye maeneo ya wananchi, likaanza kukata kata mazao. Nilipopata habari nilikwenda kujionea nikawakuta wakiendelea kuharibu mazao.

"Nilipohoji wamepata wapi kibali, wakasema 'kwa Katibu Tawala'. Kwa hiyo, tunaomba waandishi mtusaidie kupeleka kilio chetu kwa Rais wetu ambaye tunaamini kuwa suala hilo litapatiwa ufumbuzi," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema wanasikitika maeneo yao kupewa mwekezaji na wazawa kupewe viwanja au kununua, jambo ambalo wanadai ni unyanyasaji.

Uongozi wa kijiji, alidai hauna taarifa kuhusiana na mwekezaji huyo, lakini alipohoji kuhusiana na kitendo hicho cha uvamizi, aliwekwa ndani na kuelezwa kuwa uongozi wa mkoa tayari una taarifa na mwekezaji huyo.

Nafatari Chacha (70), ambaye ni mstaafu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), alisema ameishi huko kwa miaka mingi na tayari amewekeza fedha zake za kustaafu kwenye kilimo na mifugo.

Alisema kitendo cha mwekezaji huyo kuingia na kudai hicho ni lake, kumemchanganya kwa sababu fedha zake amewekeza katika kilimo na hana kazi nyingine zaidi ya kutegemea mali hizo.

"Rais atusadie kupata ardhi yetu, vinginevyo watu watakufa kutokana na mgogoro huu, lakini kwa sababu tuna imani na Rais Samia, tunaamini kuwa suala hili litapatiwa ufumbuzi wa haraka," alisema.

Hamisi Ramadhani, mmoja wa waathirika ambaye amevamiwa na kuharibiwa mazao yake, naye alimwomba Rais kuwasaidia wananchi hao wasiondolewe katika maeneo yao ya asili waliyorithi kutoka kwa wazazi wao.

"Tunamwomba Rais Samia aingilie kati mgogoro huu kwani hivi sasa tunaishi kwa hofu na hatujui huyu mwekezaji ana nia gani na sisi," alisema.

Naye Berice Makundi aliomba viongozi kuingilia katia mgogoro huu ili waendelee kuishi kwa amani bila ya hofu.

Alisema wanawake wengi katika kijiji hicho ni wakulima sasa wanapoharibiwa mazao yao watoto wao wateseka kwa njaa.

Akizungumzia mgogoro huo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alisema ulishapatiwa ufumbuzi, lakini wananchi hawakuridhika.

"Sisi tunamtambua mwekezaji huyo na tulifanya jitihada za vikao mbalimbali ili kupatikana na ufumbuzi, lakini wanannchi hawakuridhika na matokeo.

"Hivyo, kama wanaona haki yao imedhulumiwa ni vyema wakaenda ngazi za juu ili kupata haki na sisi tunatekeleza sheria tu. Kama wameona hawakutendwa haki wanapaswa kwenda mahakamani," alisema.

Naye mwekezaji anayedai eneo la kijiji hicho ni lake, Masoud Saed, alisema kampuni inayomiliki eneo hilo ina hati ya uthibitisho na kampuni iko kihalali.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# 'Familia nyingi hazina uwezo kumudu vifaa vya wanafunzi'

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KWA kutambua ugumu unaokabili wanafunzi kukidhi mahitaji yao muhimu, Taasisi ya Dido Mwanafunzi Initiative (DMI) kwa kushirikiana na Female Future Program Cohort 9 wametoa msaada wa sare za shule, madaftari na viatu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani Mtwara.

Msaada huo uliotolewa kwa Sekondari za Naliendele, Mikindani na Nanyamba pamoja na Shule za Msingi Mwenge na Mtawanya, umejumuisha taulo za kike, vesti, mabegi ya shule na vifaa vingine vya kujifunzia.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa DMI, Rehema Moses, alisema kuwa baada ya serikali kufuta ada na michango mingine shuleni, uandikishaji wanafunzi wa darasa la kwanza hata wale wanaojiunga kidato cha kwanza umekuwa mkubwa, hivyo kuibua changamoto zingine zinazohitaji ushiriki wa wadau kuzitatua.

"Serikali inajitahidi kukuza elimu nchini ila, familia nyingi haziwezi kukidhi baadhi ya mahitaji muhimu hasa ya wanafunzi kama vile sare za shule, madaftari au taulo za kike vitu ambavyo havitolewi na serikali.

"Sisi tunayo programu ya mvishe aende shule inayolenga kusaidia kutatua baadhi ya changamoto hizi. Leo tupo hapa Mtwara kesho tutakuwa mkoa mwingine," alisema Rehema.

Rais wa Female Future Program Cohort 9, Maureen Njeri, alisema kuwa wakati wanahitimu shahada ya juu katika Taasisi ya ESAMI (Eastern and Southern Africa Management Institute) mwaka 2022, waliona wanayo sababu ya kusaidia kutatua kero na changamoto wanazokabiliana nazo wanawake wenzao katika jamii, hivyo kushirikiana na DMI katika kampeni ya mvishe aende shule.

"Leo ni mwendelezo wa juhudi tunazozifanya ili kuisaidia jamii. Vifaa tulivyovitoa vimetokana na michango tunayoitoa. Ni kidogo lakini tunaamini inasaidia kupunguza tatizo.

"Iwapo wadau wengine watajitokeza, tunaweza kumaliza baadhi ya changamoto zilizopo nchini, na kuunga juhudi za serikali katika kuimarisha elimu," alisema Maureen.

Female Future Program iliyozinduliwa mwaka 2016 na Rais Samia Suluhu Hassan, kipindi hicho akiwa Makamu wa Rais, iko chini ya Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), ikisimamiwa na Shule ya Biashara ya ESAMI. Inalenga kuwezesha wanawake wengi zaidi kuingia kwenye nafasi za uongozi ili kushiriki kutoa uamuzi wa masuala mbalimbali.

"Lengo hilo halitowezekana iwapo mwanamke na mwanamume hawatoandaliwa tangu wakiwa wadogo. Elimu ndio msingi wa kila kitu ndio maana tunakwenda mpaka shule za msingi kusaidia kukuza wasichana na wavulana wenye changamoto za kijamii," alisema Maureen. Akipokea taulo za kike, Sofia Bakari, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Sekondari ya Mikindani, alisema wasichana wasio na uwezo hushindwa kuhudhuria masomo wanapokuwa kwenye siku zao, hivyo kuwapa changamoto ya kukimbizana na wenzao ili wasiachwe nyuma.

"Kuna wasichana wanaopoteza mpaka siku saba kila mwezi kutokana na hedhi. Msaada huu ni muhimu, mimi na wenzangu tulioupokea tunajua thamani yake. Tunawashukuru sana kwa kutukumbuka," alisema Sofia.



Mkurugenzi wa Dido Mwanafunzi Initiative, Rehema Moses (kushoto) na Dk. Riziki Suleiman, wakimvisha viatu mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mwenge iliyoko Kata ya Naliendele, Mtwara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilo tatu za mirungi zamponza, zampeleka gerezani miaka 30

**Na Joctan Ngelly,** MISSENYI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Missenyi, Mkoa wa Kagera imemhukumu Jamali Mussa (24), mkazi wa Bunazi wilayani hapa, kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kukutwa na dawa za kulevya aina ya mirungi kilo 3.8.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Jane Byemelwa, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Byemelwa alisema kuwa mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Alisema Upande wa Mashtaka, ukiongozwa na Inspekta wa Polisi Zakayo Napegwa, ulipeleka mahakamani huko mashahidi watano na vielelezo sita ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Byemelwa alisema mshtakiwa alikuwa anasafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi kilo 3.8 kutoka Mtukula kwenda Bukoba kwenye basi la abiria lenye namba za usajili T 980 DPZ aina ya Yutong ambayo imeandi jina Tungisi.

Alisema kuwa basi hilo linafanya safari zake Mtukula kwenda Mwanza, basi hilo lilipofika stendi ya Kyaka Wilaya ya Missenyi, askari polisi walisimamisha basi hilo na kufanya ukaguzi ndipo walipobaini mshtakiwa huyo akiwa na dawa ya kulevya aina ya mirungi kwenye begi ndogo.

Alisema mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Kyaka na alipohojiwa, alikiri kuhusika na kosa hilo na kudai kuwa dawa za kulevya alizitoa Uganda na alipeleka Bukoba kuuza.

Alisema kuwa baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika, mshtakiwa alifikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Hakimu Byemelwa alisema amesikiliza ushahidi wa pande zote na kubaini kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote na mshtakiwa inatiwa hatiani kwa kosa alilotenda.

Mwendesha Mashtaka, Inspekta wa Polisi Zakayo Napegwa alidai mahakamani kuwa hakuwa na kumbukumbu ya makosa ya nyuma ya mshtakiwa.

Aliomba mahakama itoe adhabu kali kwa kuwa kitendo alichofanya mshtakiwa cha kuchukua dawa za kulevya Uganda na kuleta Tanzania ni kibaya kwa kuwa kinapunguza nguvukazi ya vijana.

Mshtakiwa huyo alipopewa nafasi ya kuomba kupunguziwa adhabu alisema ni kosa lake la kwanza, hivyo akaomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa kuwa ana familia inamtegemea.

Hakimu Byemelwa alisema kitendo alichofanya mshtakiwa hakikubalikikatika jamii, hivyo mahakama inakuhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama zake na akimaliza kifungo, utafanya kazi halali katika jamii.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Inspekta wa Polisi Zakayo Napegwa alidai mahakamani kuwa Septemba 20, 2023, katika Kijiji cha Kyaka, Wilaya ya Missenyi, Mkoani Kagera, mshtakiwa alikutwa akiwa na dawa za kulevya aina ya mirungi kilo 3.8 kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# Bilioni 2.4/- kutumika kuboresha mtandao barabara za Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKALA wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA) wilayani Muheza mkoani Tanga umepanga kutumia Sh. bilioni 2.42 kufanyia matengenezo mtandao wake wa barabara katika mwaka ujao wa fedha.

Meneja wa TARURA wilayani Muheza, John Kwagilwa, alibainisha hayo juzi mjini hapa alipotoa taarifa ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika chini ya Mwenyekiti wa Halmashauri, Erasto Mhina.

Alisema kuwa mpango huo wa bajeti umezingatia vipaumbele vilivyotolewa na kata husika kwa kushirikiana na viongozi; madiwani na mbunge.

Meneja huyo alisema fedha zilinazoombwa katika aina hiyo ya matengenezo ni Sh. 527.91 ambazo zinatarajiwa kufanya matengenezo yenye jumla ya Km 174.44.

Alisema kuwa matengenezo ya sehemu korofi, fedha zinazoombwa ni milioni 70.81 ambazo zinatarajiwa kufanya matengenezo yenye jumla ya Km 24.31.

Alisema kuwa pia kunahitajika fungu kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum.

Meneja huyo alisema kuwa matengenezo ya madaraja, fedha zilizoombwa ni milioni 196.7, zikitarajiwa kutumika kujenga madaraja manne, makalvati 25 na mitaro mita 800.

Alisema kuwa matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami, fedha zilizoombwa ni Sh. milioni 475.

Alisema kuwa matengenezo ya barabara kwa changarawe, fedha zinazoombwa ni Sh. milioni 950 ambazo zinatarajiwa kuchonga jumla ya kilomita 22 za changarawe na barabara za kumwaga zege mita 500.

Alisema wanakabiliwa na changamoto ya fedha zinazoletwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuwa kidogo ndogo kulinganisha na mahitaji halisi.

Alibainisha kuwa mahitaji halisi mwaka huu wa fedha yalikuwa Sh. bilioni 3.395 wakati fedha zilizoidhinishwa ni Sh. bilioni 1,106 sawa na asilimia 32.6.

Alisema TARURA Wilaya ya Muheza inaomba wananchi wote kwa ujumla kutunza barabara zote ili zitumike kwa muda mrefu.

Msimamizi wa Ujenzi wa Barabara hizo, Lidya Msumari alisema kuwa ujenzi umeanza. Barabara zenye urefu wa kilomita 13.5 zimekarabatiwa.



# Ugonjwa wa ajabu waua mifugo

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

UGONJWA wa ajabu unaoathiri afya ya mifugo na kusababisha vifo kwa haraka, umeibuka katika baadhi ya vijiji mkoani Arusha, huku jamii ya wafugaji ikiomba serikali ifanye utafiti wa kubaini chanzo cha ugonjwa huo.

Baadhi ya wafugaji kutoka Wilaya ya Longido, wanadai ugonjwa huo unakumba mifugo, hasa mbuzi na kondoo, na huathiri ubongo kwa kasi hadi kusababisha vifo vingi.

Taarifa kuhusu ugonjwa huo, ilitolewa na mmoja wa wafugaji wa Wilaya ya Longido, Nambori Nabaki, mwishoni mwa wiki wakati wa jukwaa maalum lililokutanisha wadau wa kilimo ikolojia, chini ya mwavuli wa shirika lisilo la kiserikali la Island of Peace.

Akifafanua zaidi kuhusu ugonjwa huo, ambao kabila la Kimasai wameubatiza jina la 'Ormilo' Nabaki, alisema kama usipodhibitiwa kwa haraka unaweza kusababisha jamii ya wafugaji kuwa maskini katika kipindi kifupi, kwa kuwa unaenezwa na vimelea.

"Mbuzi na kondoo kule kwetu (Longido), wanakwisha kwa ugonjwa wa Ormilo. Tumejaribu kuwachinja mbuzi na kondoo kuangalia tatizo ni nini baada ya kuanguka na kufa," alisema.

Alisema mifugo iliyopata ugonjwa huo ikichingwa ubongo wao unakuwa kumejaa maji na kuiomba serikali ifanye utafiti na ipeleke wataalamu kwa ajili ya kunusuru mifugo iliyobaki isiendelee kufa.

Alisema licha ya mifugo hiyo kufa kwa ugonjwa huo tishio, bado wanakabiliana na changamoto ya uwapo wa magugu vamizi katika maeneo ya malisho yanayozuia majani ya kulishia mifugo kuota.

Kwa mujibu wa Daktari wa Mifugo wa Halmashauri ya Arusha, Linus Prosper, ugonjwa huo wa Ormilo, huwapata zaidi wanyama aina ya mbuzi, kondoo na mbwa.

Dk. Linus, ameeleza kuwa ugonjwa huo chanzo chake unatokea kwenye utumbo wa mbwa, ambapo akijisaidia kwenye majani na yakaliwa na mbuzi na kondoo, ndiko hupata maambukizi.

"Mbwa mwenye minyoo anapojisaidia kwenye majani, na binadamu akakata majani yenye kinyesi akawalisha mifugo, wanakula ile minyoo na ikiingia kwenye mifugo inabadilika kuwa lava. Hivyo, wanazaliana na mbuzi anaanza kuonyesha dalili anakuwa na kizunguzungu mpaka anakufa," alisema.

Alisema ugonjwa huo hauna dawa, bali kinachotakiwa ni kutibu minyoo kwa mbwa wote wafugwao na wanaozurura, hiyo ndio tiba pekee ya kuzuia ugonjwa huu usizidi kuenea.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mjini Babati, mkoani Manyara, Eva Makilagi Luoga (kulia), akipongezwa na wanawake wa Mtaa wa Daghailoy, Kata ya Sigino, kwa kuvishwa kitenge ili kumpa moyo kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Serikali kuboresha barabara kuvutia watalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imesema inajenga barabara ya kwenda Loliondo kwa kiwango cha lami ili kuvutia idadi kubwa ya watalii kutembelea vivutio vilivyoko ukanda wa Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha.

Meneja wa Wakala wa Barabara, Mkoa wa Arusha (TANROADS), Reginald Massawe, alisema wakala huyo anakusudia kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji.

"Loliondo haifikiki kwa lami, hivyo tumekusudia kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji. Lakini kupunguza muda wa usafiri na usafirishaji mazao na mifugo kutoka ukanda huo, hasa kwa wakazi wa Wilaya ya Ngorongoro na Mji wa Loliondo na vitongoji vyake,"alisema Massawe.

Alisema kukamilika kwa barabara hiyo, kutaongeza thamani ya mazao na mifugo na kukuza kipato kwa wananchi waishio maeneo hayo, hivyo kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii katika nchi, hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Kwa mujibu wa Meneja huyo, kwa mwaka wa fedha 2023/24, Mkoa wa Arusha, ilipokea Sh. bilioni 1 .3 kwa ajili ya kazi za dharura, zilizotokana na uharibifu wa miundombinu iliyosababishwa na mvua za El-Nino.

Aidha, alisema serikali inatambua umuhimu wa kuunganisha makao makuu ya mkoa na makao makuu ya wilaya ili

# Kanisa Katoliki lachukua hatua vijana wanaougua afya ya akili

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KANISA Katoliki nchini limeanza kuchukua hatua kunusuru idadi kubwa ya vijana waliotumbukia katika tatizo la ugonjwa wa afya ya akili katika Jiji la Arusha, linalochangia kuongezeka ukatili kwa wanandoa, ulawiti na ubakaji.

Jiji hilo limetajwa kutikisa katika miaka ya hivi karibuni, kutokana na matukio ya kikatili, yanayoziacha baadhi ya kaya katika simanzi na majonzi makubwa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Ulinzi na Usalama wa Watoto wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Padri Dennis Ngowi, alisema dalili za kuongezeka kwa matukio ya aina hiyo, ni aina ya watu wanaoendelea kutoa kauli za vitisho kwa Watanzania wenzao.

Padri Ngowi alisema kwa sasa jamii ya wakazi wa Arusha, inapaswa kuchukua hatua kwa kutambua watu wanaonyemelewa na dalili za magonjwa ya afya ya akili, ikiwamo wale wanaosahau mambo na kutamka maneno ya vitisho.

"Tatizo la afya ya akili linasababishwa na mfumo wa maisha, malezi na makuzi na kutowajibika kwa jamii ipasavyo. Tumeanza kama kanisa kuchukua hatua kudhibiti tatizo hili tangu dalili za awali zinapoanza, badala ya kufikiria kwamba mambo haya yanachagizwa na ushirikina," alisema Padri Ngowi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, taasisi hiyo imejikita katika kumtetea mtoto, kwa sababu hawezi kujisemea tofauti na mtu mzima, ambaye anaweza kutoa taarifa anapoona anatendewa kinyume cha matakwa yake.

Aidha, alisema taasisi hiyo kwa sasa imeanza imekuwa kutoa elimu kupitia semina za wanafunzi katika shule za msingi na sekondari na vikao vya wazazi vya kila mwezi katika siku maalum za wazazi kutembelea watoto shuleni.

"Elimu imezaa matunda na kuleta matokeo chanya kwa kuibua watu wanatenda au kutendewa mambo kinyume na maadili, lakini bado kazi hii inajitaji watu wengi ili wapokee elimu itakayoenezwa kwa wigo mpana," alisisitiza Padri Ngowi.

"Utamsikia mzazi anasema mtoto wangu hawezi kupitia shida nilizopitia, nitampa kila kitu atakachotaka. Mara mtoto hazeeki kwa mzazi nitakaa naye, kijana huyo atajitambua na kujua kwamba anatakiwa kubeba majukumu ya familia lini?

"Wazazi kulea imekuwa ni tatizo kubwa; niseme kwa asilimia kubwa wazazi wanachangia vijana wa kike na kiume kuwa mfano mbaya usiyofaa kuigwa katika jamii kwa sababu ya malezi mabaya kutoka kwa wazazi wao."





## Maji yatajwa kuua 14 Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATI ya vifo 24 vilivyotokana na matukio mbalimbali mkoani Shinyanga kwa mwaka 2023, 14 vimetajwa kutokana na watu kusombwa na maji.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Shinyanga, Martin Nyambala, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kutoa taarifa ya matukio yaliyotokea mwaka jana.

Alisema kwa kipindi hicho yalitokea matukio yasiyozidi 80, ambako kati ya hayo matukio ya moto majumbani yalikuwa 29, taasisi na biashara 18, miundombinu ya umeme 10, ajali barabarani saba na ajali za maji 13.

Alitaja vifo vilivyotokea kufuatia matukio hayo kuwa ni 24 huku majeruhi wakiwa 41 ambako kati ya vifo hivyo 24, 14 vilitokana na watu kusombwa na maji 14 kwenye mito.

"Wengine watano walifariki dunia kwa ajali ya moto na waliosalia watano walifariki dunia katika matukio mengine zikiwamo ajali za barabarani," alisema Nyambala.

Alitoa wito kwa wananchi kuwa makini na mvua ambazo zinaendelea kunyesha kwa kutovuka kwenye mito iliyojaa maji na kuzuia pia watoto wao wasiende kuogelea wala kuvua samaki kwenye mito hiyo.

Alitahadharisha pia wakazi wanaoishi mabondeni na kwenye mikondo ya maji wahame ili kunusuru maisha yao. Katika hatua nyingine, Nyambala alitaka wananchi kuwa makini na matumizi ya nishati majumbani ikiwamo gesi pamoja na jiko mkaa, kwamba wanapopikia ndani wahakikishe madirisha yanakuwa wazi, ili kupitisha hewa na kuwa salama wakati wa matumizi.

Alielekeza wafanyabiashara kuhakikisha wana vifaa vya kuzimia moto ili waudhibiti unapoanza kuwaka wakati Jeshi hilo likiwa njiani kuwaongezea nguvu ili kunusuru vitu na watu.

Baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Shinyanga, waliomba jeshi hilo kuwa na utaratibu wa kutoa elimu mara kwa mara kwa wananchi, namna ya kuepukana na majanga ya moto ambayo yanatokana na uzembe, pamoja na jinsi ya kuuzima moto kwa hatua za awali.



Mwakilishi wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, William Chungu, akiongea katika hafla ya kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa sekondari wilayani Msalala mkoani Shinyanga yaliyomalizika mwishoni mwa wiki wilayani humo kwa ufadhili wa Barrick Bulyanhulu. Jumla ya walimu 336 walihudhuria mafunzo hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wasiolipia chakula wadaiwa kufungiwa darasani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wa shule za msingi na sekondari katika Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, ambao wazazi wao wameshindwa kulipia chakula na mitihani ya kila mwezi, wanadaiwa kufungiwa darasani ili wasirejee nyumbani kwao kula.

Utaratibu huo unadaiwa upo kwa muda mrefu na wazazi wanapohoji, huambiwa wahamishie watoto wao katika shule zisizokuwa na michango ya aina yoyote.

Hayo yalibainishwa juzi na baadhi ya wazazi na walezi katika mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika sekta ya afya, elimu, maji, kilimo, ardhi na miundombinu ya barabara uliofanyika katika Kata ya Majengo.

Mmoja wa wazazi, Ruben Macheyeki alisema, wanafunzi wa darasa la kwanza, pili, tatu, tano na sita wanatakiwa kutoa Sh. 5,000 ya uji kila mwezi huku wanafunzi wa madarasa yenye mitihani ya darasa la nne na saba wanatozwa Sh. 3,000 ya mitihani ya mwezi na Sh. 3,500 ya chakula cha wiki. "Siku za mitihani kwa wanafunzi ambao hawajatoa fedha za mitihani huchapwa bakora na kuwaaguza watuambie tuwahamishie shule ambazo hazina michango, suala hili limekuwa likituchonganisha na watoto wetu wakituona hatuwajali kabisa," alisema Macheyeki.

Salome William alisema wanafunzi wa sekondari kila mmoja anachangishwa kilo 15 za mchele, saba na nusu za maharage na Sh.10,000 kwa ajili ya malipo ya mpishi pamoja na ununuzi wa kuni za kupikia.

Aliiomba serikali iingilie kati ili watambue uhalali wa michango hiyo kwa wote wanahitaji watoto wao wasome.

Akijibu malalamiko hayo, Ofisa Elimu Msingi Hamida Kaganda alisema, suala la chakula shuleni ni lazima na linapangwa baina ya wazazi na bodi za shule kwa viwango vinavyotakiwa kutolewa.

Aidha, alisema hana taarifa ya michango mingine na kuahidi kufuatilia na kuchukua hatua kwa wanaofanya hivyo.

Ofisa Elimu Sekondari, Anastazia Manumbu alisema, alifuatilia malalamiko hayo na kubaini Sekondari ya Kishimba ndio inayochangisha michango ya fedha za mitihani ya kila mwezi kwa madarasa yenye mitihani.

Aliahidi kukutana na wakuu wa shule na wazazi kujadili na kutatua kwa pamoja changamoto hiyo.

Mkuu wa Mkoa huo, Christina Mndeme, aliwaagiza maofisa elimu wa shule za msingi na sekondari, walimu wakuu, wazazi pamoja na maofisa elimu kata kukaa kwa pamoja na kutatua malalamiko hayo, kwani serikali imepiga marufuku michango isiyokuwa na tija kwani inaumiza mzazi.

# Vijiji 20 Tabora kufikiwa maji toka Ziwa Victoria

**Na Halima Ikunji,** TABORA

VIJIJI 20 vya Tarafa ya Bukene, Wilaya ya Nzega mkoani Tabora vinatarajiwa kunufaika na mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria unaosimamiwa na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Naitapwaki Tukai, wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye Kata na Kijiji cha Uduka na kusema kuwa mradi huo umefikia asilimia 25.

Alisema mradi huo utawafikia jumla ya wananchi 85,607 katika halmashauri hiyo na kuwataka wananchi hao kuitunza miundombinu hiyo kwa kuwafichua wahalifu ili sheria ichukue mkondo wake. Alisema katika upanuzi wa mradi huo maji yataenda katika Vijiji vya Shila, Shigamba, Kagongwa, Itobo, Lakuyi, Chamwabo, Bukene, Kabanga, Uduka, Ussongwanhala, Kayombo, Mwamala, Kashili, Seki Chaming'hwa , Kasela, Senge Lububu, Nindo na Udutu. Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Nzega, Mhandisi Faustine Makoka, alisema upanuzi wa mradi huo unatarajiwa kukamilika Oktoba 23 mwaka huu, ukigharimu Sh. bilioni 24 .

Alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa matangi matatu yenye ujazo wa lita 150,000, milingoti tisa na tangi moja lenye ujazo wa lita 150,000 usawa wa ardhi ambako ukikamilika wananchi watanunua maji kwa Sh.20.

"Kutakuwa na ujenzi pia wa matangi 2 yenye ujazo wa lita 100,000 kwenye milingoti 12, tangi moja lenye ujazo wa milimita za ujazo 100,000 vichotea maji 12 pamoja na uchimbaji wa mitaro wenye urefu wa mita 193,502," alisema. Alisema ujenzi huo unatekelezwa kupitia mpango wa programu kwa matokeo ya PforR na tayari Sh. bilioni 4.3 zimetumika.

Nipashe
Spotika



NYOTA 10 WATAKAOWINDWA SAUDIA MSIMU HUU WA JOTO UK. 12-13



# WALINZI WA KATI BORA ZAIDI WAKIHISTORIA EPL

VIRGIL VAN DIJK

**LONDON,** England

BAADA ya kufunga bao la ushindi na kunyanyua Kombe la Carabao Jumapili, Virgil van Dijk ameimarisha hadhi yake ya kuwa mmoja wa mabeki bora kabisa wa Ligi Kuu England kuwahi kutokea.

Mholanzi huyo amekuwa na mchango mkubwa katika kumsaidia kocha Jurgen Klopp kushinda kila kitu alichopewa wakati alipokuwa hapo Merseyside.

Hapa tunawaangalia walinzi wa kati bora zaidi katika historia ya Ligi Kuu England, twende sasa...

**#5. Tony Adams**

Aliitwa Bwana Arsenal kwa juhudi zake pale Kaskazini mwa London. Tony Adams anabakia kuwa mchezaji pekee kuwa nahodha wa timu iliyoshinda mataji ya ligi katika miongo mitatu tofauti.

Beki huyo zao la akademi ya klabu hiyo alikuwa gundi akishikilia mambo pamoja na Arsene Wenger mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000 - na mapenzi yake kwa mchezo yalipamba moto katika uchezaji wake.

England haijatoa mabeki wengi wa jadi bora zaidi ya Adams, ambaye atakumbukwa daima kwa bao lake dhidi ya Everton mnamo Mei 1998 ambalo lilisaidia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England.

**#4. Vincent Kompany**

Vincent Kompany ndiye gwiji mkubwa wa Manchester City na ndiye aliyewaongoza katika zama zao mpya.

Utumishi wake pale Etihad ulimfanya kushinda tuzo kuu 12 na haishangazi kwamba klabu iliamua kujenga sanamu yake nje ya uwanja.

Majeraha yalizuia kazi ambayo inaweza kuwa ya utukufu zaidi, lakini Kompany bado bila shaka ni mmoja wa magwiji wa zama za kisasa.

**#3. Virgil van Dijk**

Kurejea kwa Liverpool kileleni kulilingana na kuwasili kwa Van Dijk pale Merseyside Januari mwaka 2018.

Mchezaji huyo wa Uholanzi alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mechi katika fainali tatu kuu za 'Wekundu' hao - ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya- na hakubahatika kushinda Ballon d'Or mnamo 2019.

Tangu kutwaa taji la ligi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30, Van Dijk amekuwa akipata kutambuliwa na atakuwa na nia ya kushinda medali zaidi kabla ya msimu wa 2023-24 kukamilika.

**#2. Rio Ferdinand**

Rio Ferdinand alikuwa na kazi nzuri na ingawa heshima yake kuu ilipatikana akiwa na Manchester United, alikuwa bora wakati wake Leeds United na West Ham.

Kama Van Dijk, Ferdinand alifaa kama beki wa kati wa kisasa na alikuwa na mchanganyiko mzuri wa nguvu, kasi na ufundi, na kumruhusu kuweka nafasi yake chini ya Alex Ferguson kwa zaidi ya muongo mmoja.

Ushirikiano wake na Nemanja Vidic ulikuwa muhimu kwa mafanikio ya United katika karne ya 21 na Muingereza huyo hatimaye aliachana na soka na baada ya kunyakua mataji sita ya Ligi Kuu England.

**#1. John Terry**

Tukiwa na rekodi ya ushindi ya zaidi ya asilimia 60 kwenye ligi, haishangazi kumuona nguli John Terry akiongoza orodha yetu kama beki wa kati bora zaidi wa Ligi Kuu England.

Gwiji huyo wa Chelsea alikaa kwa miaka 19 huko London Magharibi na alishinda tuzo kuu 15, pamoja na mataji matano ya Ligi Kuu, matano ya Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hadhi yake kama nyota inaungwa mkono na ukweli kwamba ana safu safi zaidi ya beki yeyote katika historia ya Ligi Kuu na pia ndiye beki aliyefunga mabao mengi zaidi kwenye mashindano.

## ISIKUPITE

MABAO 27 ya mipira ya kutenga (set-piece goals) ambayo Arsenal imefunga hadi sasa msimu huu (ikiwa ni pamoja na penalti 8) ndio rekodi yao kubwa zaidi kwa msimu mmoja wa ligi tangu Opta ilipoanza kurekodi data kama hizo mnamo msimu wa 2004-05.



# NYOTA 10 WATAKAOWINDWA SAUDIA MSIMU HUU WA JOTO

**LONDON,** England

MAPINDUZI ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, siyo tu yameweza kuvutia baadhi ya nyota wakubwa wa soka wa nyakati za kisasa, lakini magwiji wa muda wote.

**Cristiano Ronaldo alianzisha hilo huko Saudi Arabia, huku watu kama Karim Benzema na Neymar wakifuata nyayo zake.**

Matarajio makuu ya Ufalme yameifanya Saudi Pro League (SPL), kupata umaarufu mkubwa, na hakuna dalili za nchi hiyo kupunguza matumizi yao hivi karibuni kabla ya uwezekano wa kuandaa Kombe la Dunia mwaka 2034.

Wachezaji wa Ulaya wakubwa wanatafutwa na kuna angalau majina kumi ya nyota wapo kwenye rada. Hapa tunawaangalia wachezaji 10 ambao watawindwa na Ligi Kuu ya Saudi Arabia wakati wa majira ya joto, twende sasa...

### #1. Kevin De Bruyne (Manchester City)

Kevin De Bruyne atakumbukwa kama mmoja wa viungo bora wa muda wote wa Ligi Kuu England na Mbelgiji huyo sasa ameingia kwenye rada za Saudia kutokana na hali ya mkataba wake pale Man City.

Mkataba wa sasa wa Mbelgiji huyo kule Etihad unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, na mazungumzo kuhusu kuongeza muda bado hayajapamba moto. Man City, bila shaka, hawatataka kumpoteza supastaa wao bure iwapo atachagua kutoongeza mkataba mpya, huku klabu hiyo ikiripotiwa kuweka bei ya pauni milioni 90 kwenye kichwa cha De Bruyne.

Utajiri wa Saudi unamaanisha kuwa hesabu kama hiyo haitatumika kama kizuizi. De Bruyne atakuwa mapinduzi mengine makubwa kwa soka la Saudi Arabia.

### #2. Raphael Varane (Manchester United)

Ingawa Varane ameonesha bado ana uwezo wa kushindana kwa kiwango cha juu zaidi pale Manchester, wakati wake kule United umekuwa wa kushangaza sana.

Mkataba wa Mfaransa huyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na ingawa kuongezwa kwa masharti yaliyopunguzwa hakujaondolewa, Varane anatazamiwa kujikuta akipewa ofa nono kutoka Saudia.

Al Nassr na Al Ittihad ni klabu zinazotaka kumsajili beki huyo wa kati kwa uhamisho wa bure msimu huu wa majira ya joto Al Ittihad ya Benzema iko tayari kumpa Varane mshahara wa thamani ya euro milioni 30 kwa msimu.

### #3. Luka Modric (Real Madrid)

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alionesha kuwa bado ana kipaji kikubwa kwenye mchezo dhidi ya Sevilla wiki iliyopita akifunga bao pekee. Hata hivyo, Modric amekuwa na jukumu dogo tu kwa Real Madrid msimu huu, na wengine wamebashiri kwamba anaweza kustaafu.

Kutokana na wasifu wake, kiungo huyo alishawahi kuzivutia klabu za SPL. Hata hivyo, wakala wake alifungua mlango wa kuhamia Saudia Novemba mwaka jana na kupendekeza kwamba "ofa inayofaa" itazingatiwa ikiwa itafika.

### #4. Romelu Lukaku (Roma, kwa mkopo kutoka Chelsea)

Romelu Lukaku aliyecheza jumla ya mechi 113 kwa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, anaonekana kujiandaa kwa malipo makubwa huko Mashariki ya Kati.

Lukaku aliwahi kukataa kuhamia Al Hilal, lakini kuhamia SPL inaonekana kuwa suala la muda tu. Bila shaka atapata maslahi mengi kutoka kwa Saudia msimu huu wa majira ya joto, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, hivi majuzi alidai kuwa SPL ina uwezo wa kuwa "mojawapo ya ligi bora zaidi duniani."

Lukaku pia alijibu "kabisa" alipoulizwa ikiwa mashabiki wa Saudia wangemwona tena mshambuliaji huyo Mashariki ya Kati siku moja. Kwa sasa yuko kwa mkopo katika Klabu ya Roma na huenda akahama mwishoni mwa msimu huu.

### #5. Mohamed Salah (Liverpool)

Uamuzi wa Jurgen Klopp kuondoka Liverpool mwishoni mwa msimu umeonekana kutia shaka mustakabali wa nyota wakuu wa klabu hiyo.

Virgil van Dijk na Salah walihusishwa kwa haraka na kuondoka baada ya tangazo la Klopp.

Salah yuko chini ya mkataba na Liverpool hadi 2025, kumaanisha hali yake ni sawa na ya De Bruyne. 'Wekundu' hao bila shaka, hawatataka kumpoteza supastaa wao, lakini watajihatarisha kumruhusu Salah kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake ikiwa mazungumzo ya kuongeza muda hayajaendelea.

Kwa kuzingatia umri wake na labda msimu huu wa majira ya joto ndio wakati muafaka wa kuachana na Mmisri huyo. Wasaudia kwa muda mrefu wamekuwa wakihangaikia kumtunuku nyota huyo.

### #6. Casemiro (Manchester United)

Casemiro alivutia wakati wa msimu mzuri wa Manchester United msimu wa 2022/23, lakini kampeni ya sasa imekuwa ngumu kwake.

Mbrazil huyo amekosa sehemu yake kubwa kutokana na jeraha lakini pia amekuwa na shida ya kucheza akiwa fiti. Kwa hiyo, kutokana na mabadiliko makubwa yanayotokea Old Trafford, United inaweza kumuondoka kiungo huyo mkongwe msimu huu wa majira ya joto.

Wakati kiungo huyo amesisitiza kuwa ana furaha pale Manchester, uamuzi kuhusu mustakabali wake msimu huu unaweza kuwa nje ya udhibiti wake. Iwapo atasonga mbele, SPL bila shaka ndiyo mahali anapoelekea zaidi.

### #7. Thomas Partey (Arsenal)

Thomas Partey amekuwa na wakati mgumu msimu huu. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ghana amekuwa nje ya uwanja tangu mapumziko ya Oktoba mwaka jana baada ya kufanyiwa upasuaji wa paja. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30, anatazamiwa kurejea hivi karibuni.

Wakiwa wamemsajili Declan Rice majira ya joto yaliyopita, Arsenal watajaribu kuimarisha safu yao ya kiungo zaidi mwishoni mwa msimu huu - Martin Zubimendi na Douglas Luiz ni miongoni mwa wanaohusishwa na kuhamia Emirates.

Partey anaweza kutolewa ili kutoa nafasi kwa wachezaji wapya wa safu ya kati. Juventus wamekuwa wakihusishwa kwa muda mrefu, kama ilivyo kwa Al Ahli.

### #8. Son Heung-min (Tottenham Hotspur)

Nyota huyo wa Korea Kusini alipata ofa kutoka Saudia baada ya kampeni ya msimu wa 2022/23. Son alifunga uhamisho wa kuelekea Mashariki ya Kati msimu uliopita wa majira ya joto na tangu wakati huo amefurahia kampeni ya kurejea Tottenham Hotspur huku Ange Postecoglou akishikilia usukani.

Klabu za Saudia zinatazamiwa kufufua nia yao ya kumnunua nahodha huyo wa Spurs msimu huu wa majira ya joto. Umashuhuri wa Son katoka mashariki ya mbali unamaanisha kuwa angekuwa mapinduzi makubwa kwa mradi wa Saudia, lakini kuondoka hivi karibuni pale Spurs kunaonekana kutowezekana.

Tottenham wana chaguo la kuongeza mkataba wa nahodha wao kwa mwaka mmoja zaidi ambao utamweka Kaskazini mwa London hadi 2026.

### #9. Bruno Fernandes (Manchester United)

Imekuwa kampeni tulivu sana ya 2023/24 kwa Bruno ambaye ni moyo wa ubunifu wa United, ambao waliripotiwa kukataa ofa kutoka Saudi Arabia Januari,

Fernandes amekuwa akipata fedha nyingi sana kwa 'Mashetani Wekundu' tangu alipojiunga na klabu hiyo kutoka Sporting CP mwaka 2020. Tayari tumegundua uwezekano wa Varane na Casemiro wa United kujiunga na mapinduzi ya Saudia majira ya joto, na Fernandes anaweza kulengwa tena.

Mchezaji huyo wa Ureno hakushawishiwa na ofa ya Al Hilal wakati wa majira ya baridi kali, na Fernandes anasisitiza kwamba bado ana mengi ya kufanikiwa katika soka la Ulaya.

### #10. Thiago (Liverpool)

Mhispania huyo ambaye alisaini mkataba wa miaka minne baada ya kusajiliwa na Liverpool mwaka 2020 na bado hajasaini nyongeza, hajashiriki katika kipindi hiki na siku zake zinahesabika pale Merseyside.

Matatizo ya mara kwa mara ya majeraha yanamaanisha kuwa kuna uwezekano mdogo wa kuongezwa muda.

Hilo linafungua mlango wa kuhamia Saudi Arabia, ingawa mchezaji huyo alikataa kuhamia wakati wa msimu wa majira ya joto.




## Nukuu

"Asilimia 100, Mo Salah bila shaka ataondoka msimu huu wa majira ya joto. Haijalishi nini kitatokea msimu huu - nadhani kulikuwa na makubaliano msimu uliopita." Ataondoka na kucheza mahali kama Saudi Arabia, na natumai, Liverpool watapata ada kubwa na kupata wachezaji kadhaa kutoka nyuma yake. Salah atakuwa mfalme nchini Saudia," **Nguli wa Liverpool, Mark Lawrenson, akiweka wazi Mohamed Salah ataondoka mwishoni mwa msimu.**



"Hiyo ni kama kubwa ambayo nimewahi kuhisi kwa sababu kufunga kila kitu kwa klabu ya aina hii, Barcelona. Ninajivunia na nina furaha sana. Na ninatumai kwamba idadi hii itakua kwa kasi sana na hata zaidi," **Mshambuliaji wa Barcelona, Robert Lewandowski baada ya kufikisha mabao 50 katika klabu hiyo aliyojiunga nayo 2022. Lewa amefikisha idadi hiyo baada ya mechi 79 huku akiwa na asisti 14.**



"Nitakuwa na wasiwasi ikiwa hatufungi mabao mengi, ikiwa hatutengenezi nafasi, ambayo ni kinyume, nadhani tunatengeneza sana, tunafunga mabao mengi. Mpango ni kwa kila mwaka kujaribu kuwa bora, nadhani tuko katika wakati mzuri na tuone kama tunaweza kuendelea kuboresha," **Mkurugenzi wa Michezo wa Arsenal, Edu, akikiri kwamba anaelewa kwa nini mashabiki wanaitaka timu kusajili mshambuliaji.**





Kipa wa Jwaneng Galaxy, Goitseone Phoko na nahodha wake, Tlamelo Kolagano, wakishindwa kuzuia moja ya mabao sita yaliyofungwa, huku mfungaji wa bao la pili, Pa Omari Jobe akishuhudia mpira ukijaa wavuni, katika mechi ya hatua makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Simba ikishinda mabao 6-0 na kufuzu hatua ya robo fainali. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI 5 TAMU, SIMBA, YANGA ROBO FAINALI CAF

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 6-0 ilioupata dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana juzi usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, umeifanya Simba kuungana na Yanga kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba imekuwa ni timu ya pili nchini kutinga hatua hiyo baada ya Yanga, kufanikiwa kufanya hivyo, Februari 24, mwaka huu ilipoitandika CR Belouizdad ya Algeria mabao 4-0, kwenye uwanja huo huo.**

Katika makala haya, tunakuletea rekodi na takwimu za timu hizo na wachezaji wake hadi zinatinga hatua hiyo ya robo fainali.

### 1. Simba, Yanga zaitisha Afrika

Simba na Yanga zimeweka rekodi ya kuwa timu mbili pekee msimu huu kutoka nchi moja kutinga hatua ya robo fainali msimu huu.

Simba imetinga kutoka Kundi B, ikishika nafasi ya pili, huku Yanga ikishika pia nafasi kama hiyo kutoka Kundi D.

Rekodi hii inaifanya Tanzania kwa mara ya kwanza kuwa na timu mbili kwenye hatua hiyo.

Nchi zingine zimeingiza timu moja moja ambazo ni Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini, na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kutoka Kundi A, Asec Mimosas ya Ivory Coast kutoka Kundi B, Petro de Luanda ya Angola na Esperance ya Tunisia kutoka Kundi C na Al Ahly ya Misri kutoka Kundi D.

### 2. Simba mara nne, Yanga moja

Wakati Yanga ikitinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa mara ya nne, Yanga imefanya hivyo mara moja tangu kuanza kwa mfumo mpya wa ligi hiyo 1997.

Simba imefanya hivyo msimu wa 2018/19, 2020/21, 2022/23 na msimu huu wa 2023/24, huku ikiweka rekodi nyingine ya kucheza hatua hiyo mara mbili mfululizo kwani msimu uliopita ilifikia hatua hiyo na kutolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.

### 3. Zote zimefunga mabao tisa

Timu zote zimefunga mabao tisa mpaka zinamaliza hatua ya makundi. Yanga ilipata mabao yake ilipotoka sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Al Ahly, sare nyingine kama hiyo dhidi ya Medeama Ghana ugenini, ikaiadhibu Medeama nyumbani mabao 3-0, kabla ya kuiangamiza CR Belouizdad mabao 4-0.

Simba ilianza kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Asec Mimosas nyumbani, ikaifunga Wydad Casablanca mabao 2-0, kabla ya kuishindilia Jwaneng Galaxy mabao 6-0.

### 4. Simba wageni sita, Yanga wanne

Wachezaji wa kigeni sita wamehusika kufunga mabao hayo kwa upande wa Simba, huku Yanga yakiwa yamefungwa na wachezaji wanne.

Mabao ya Simba yalifungwa na Mrundi Saido Ntibanzonkiza, aliyepachika mawili, na Willy Onana raia wa Cameroon pia akiweka mawili kwenye kamba.

Waliofunga nao moja moja ni Mzambia Clatous Chama, Mkongomani, Fabrice Ngoma, na Mgaboni Pa Omari Jobe. Kwa maana hiyo, wachezaji wa kigeni wa Simba wamechangia jumla ya mabao saba.

Pacome Zouzoua, raia wa Ivory Coast, amewaongoza wageni wa Yanga kupachika mabao matatu peke yake, mengine yakifungwa na Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki, Mzambia, Kennedy Musonda na Joseph Guede ambaye ni pia ni wa Ivory Coast, wote wakifunga bao moja kila mmoja.

Hii inaonyesha kuwa upande wa Yanga, wachezaji wa kigeni wamefunga mabao sita kwenye hatua hiyo ya makundi.

### 5. Watanzania wawili wawili

Wachezaji wawili wa Kitanzania kwa kila timu wamechangia mabao hayo kwa timu zao. Wakati kwa upande wa Simba wakichangia mabao mawili, Yanga ina mabao matatu ambayo yamechangiwa na wazawa.

Kibu Denis na Ladaki Chasambi juzi walifunga mabao, wakiwa ni moja ya wauaji wa Jwaneng Galaxy, huku Mudathir Yahaya akifunga mabao mawili upande wa Yanga na Bakari Mwamnyeto.

## JE, WAJUA?



KATIKA msimu huu wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Tanzania imeweka rekodi ya kuwa nchi pekee iliyofanikiwa kuingiza timu mbili hatua ya robo fainali; Simba na Yanga, nchi zingine zote zimeingiza timu moja moja. Rais Samia amekuwa akitoa motisha wa Sh. milioni tano kwa kila bao linalofungwa na timu kushinda kwa klabu hizo kwenye mechi za kimataifa.





# Serikali kuwekeza nguvu matumizi teknolojia shuleni

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuweka nguvu kwenye matumizi ya teknolojia katika kutoa elimu shuleni, ili kukabiliana na upungufu wa walimu nchini.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde, aliyasema hayo jana jijini hapa alipotembelewa na ujumbe wa wataalamu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Wajumbe hao pia walifanya ziara Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ili kujifunza namna tume hiyo inavyotekeleza majukumu yake.

Dk. Msonde alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali za kuboresha elimu ili kuhakikisha kila mwanafunzi anapata elimu kama inavyohitajika.

"Kwa sasa tumeanza majaribio ya matumizi ya teknolojia ya ufundishaji inayowezesha mwalimu kutoka kituo kimoja kufundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja wakiwa katika maeneo mbalimbali. Tumeanza katika mikoa ya Pwani na Dodoma na matokeo yake ni mazuri, wanafunzi wanafurahia," alisema Dk. Msonde.

Aliongeza kuwa, "kupitia teknolojia hiyo mwalimu anaona wanafunzi wake wote katika maeneo mbalimbali, anaweza kuuliza swali na mwanafunzi akanyoosha mkono na kujibu, yaani ni kama mwalimu yupo hapo hapo."

Alifafanua kuwa mfumo huo pamoja na kurahisisha utendaji kazi kwa walimu, ni moja ya njia za kukabiliana na upungufu wa walimu hususani wa masomo ya sayansi na hisabati.

"Katika kuendeleza jitihada hizi, Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa tayari ameagiza kutengwa kwa bajeti ili kuwezesha upatikanaji wa angalau darasa moja kwa kila mkoa na kila halmashauri katika mwaka wa fedha 2024/25," alisema.

Pamoja na hayo, Dk. Msonde alieleza kuwa TSC inaendelea kusimamia masuala ya utumishi wa walimu kwa ufanisi ikiwamo ajira, maadili na maendeleo ya walimu.



Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, David Mashauri, akikagua vyoo viwili vyenye matundu 12 na chumba maalumu cha kujistiri, vilivyojengwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Shinyanga katika Shule ya Sekondari Busiya wilayani humo juzi. Kushoto mwenye miwani ni Meneja wa TCB Tawi la Shinyanga, Julius Mataso. **PICHA: MARCO MADUHU**

# CCM yaingilia kati malori kuegeshwa kituo cha mabasi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida kimeishauri serikali kuondoa utaratibu wa malori kuegeshwa katika kituo cha mabasi Manyoni kwa kuwa unahatarisha usalama wa abiria.

Mwaka jana serikali ya Mkoa wa Singida ilitoa agizo kwamba malori yaegeshwe usiku katika stendi hiyo ili halmashauri ipate mapato badala ya awali ambapo yalikuwa yanaegeshwa kandokando mwa barabara.

Mwenyekiti CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea kituo hicho na kupokea malalamiko kwa wananchi kuwa uwapo wa malori na mabasi eneo hilo unahatarisha usalama wao. Alisema sio jambo jema kwa mabasi na malori kuegeshwa katika kituo hicho ambacho kilitengwa kwa ajili ya mabasi na kuiagiza halmashauri itafute eneo jingine kwa ajili ya malori ili kuleta usalama kwa watumiaji.

Baadhi ya watumiaji wa kituo hicho walisema kutokana na hali hiyo baadhi ya mabasi yamekuwa yakipitiliza bila kuingia ndani ya kituo na wakati mwingine kushusha abiria nje ya kituo.

Hata hivyo waliiomba serikali kuwasaidia kutatua tatizo hilo la malori kwa kuwa yamekuwa yakiharibu stendi hiyo kutokana na uzito wa mizigo yanayobeba.

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ulisema wanaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha wanatenga eneo jingine ambalo malori hayo yatakuwa yanapaki.

Ziara hiyo ya Kamati ya Siasa Mkoa wa Singida ilitembelea Kituo cha Afya Kata ya Sanza, baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo waliishukuru serikali kwa kuendelea kutekeleza miradi ambayo inawaondolea wananchi adha ya kufuata huduma za afya na kijamii umbali mrefu.

# BMH yapandikiza betri wagonjwa watatu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) imefanya upandikiza betri kwenye moyo kwa wagonjwa watatu wenye matatizo ya moyo.

Upandikizaji wa betri kwenye moyo ambao kitaalamu unaitwa 'pacemakers' implantation' unafanyika kwa watu wenye matatizo ya mfumo wa umeme wa moyo na kusababisha mapigo ya moyo kuwa chini ya kiwango.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Idara ya magonjwa ya Moyo, Dk. Happiness Kusima alisema kinachotakiwa kwa mtu wa kawaida ni mapigo ya moyo kuwa ni 60-100 kwa dakika lakini wengi wa wagonjwa wenye matatizo hayo mapigo yao ni chini ya 40.

Dk. Kusima alisema kuwa hospitali hiyo hadi sasa imepandikiza huduma hiyo kwa watu 18 tangu ianzishwe mwaka 2021.

"Jana tumepandikiza watu watatu na kupelekea idadi ya wagonjwa wenye matatizo ya moyo, kufikia 18 toka huduma hiyo ianzishwe mwaka 2021," alisema Dk. Kusima.

Alifafanua kuwa upandikizaji huo umefanyika kwenye kambi ya Madaktari Bingwa wa Moyo wa BMH kwa kujengewa uwezo na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ya jijini Dar es Salaam.

Alitoa wito kwa wagonjwa wenye matatizo hayo kujitokeza hospitalini hapo kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu.

Alisema hivi sasa huduma hiyo hupatikana katika hospitali hiyo kutokana na kuwa na kambi ya madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo ambao wamejengewa uwezo wa utoaji wa matibabu hayo.

"BMH inafanya matibabu ya upasuaji wa moyo pamoja na matibabu ya magonjwa mengine mbalimbali jambo lililosaidia kuwapunguzia wagonjwa kwenda umbali mrefu kutafuta huduma ya matibabu ya moyo," alisema.

Aliishukuru serikali kwa kufanya uwekezaji katika sekta ya afya ambao yamechangia kwa kiasi kikubwa huduma za matibabu mbalimbali kupatikana katika hospitali hiyo.



## HABARI MBEYA

# Madaktari wabaini chanzo wanafunzi kupoteza usikivu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wanafunzi mkoani Mbeya, wamebainika kuwa na vitu visivyokuwa vya kawaida kwenye masikio ikiwamo vijiti, pamba na mbegu za mazao mbalimbali yakiwamo maharage hali inayosababisha kupoteza usikivu.

Aidha baadhi ya wanafunzi hao wamebainika kuwa na tatizo la nta kuganda masikioni pamoja na maambukizi sugu yanayosababisha ngoma ya sikio kutoboka na kutoa usaha mara kwa mara na hivyo kuhatarisha usikivu wao.

Madaktari bingwa wa masikio, pua na koo walibaini hayo walipotembelea shule mbalimbali jijini Mbeya kwa lengo la kuwapima usikivu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya usikivu duniani ambayo kilele chake ilikuwa jana.

Dk. Libason Hosea alisema watu wengi hupuuza matatizo ya masikio hasa tatizo la kutoa usaha sikioni wakidhani ni hali ya kawaida hali ambayo huathiri usikivu wao.

Aliwashauri watu wote wenye matatizo ya usikivu kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili wachunguzwe na kufanyiwa matibabu mapema kabla ya matatizo hayajawa makubwa zaidi.

"Tumewashauri watoto kuacha kutumia vijiti, pamba au vitu vyovyote vya kusafisha masikio kwa sababu vitu hivyo ni hatari vinasababisha kutoboa ngoma ya sikio, sikio halihitaji kusafishwa, sikio linajisafisha lenyewe," alisema Dk. Hosea. Alisema mwanafunzi aoteza usikivu inaweza kumrudisha nyuma kielimu na kwamba baadhi ya wazazi hawafahamu kuwa watoto wao wana matatizo ya usikivu.

Alisema baadhi ya wazazi huwa wanawaadhibu watoto wao wanapowaelekeza vitu na kukuta wanafanya tofauti wakidhani ni makusudi kumbe wanakuwa hawawasikii kutokana na usikivu hafifu.

Awali akizungumza na madaktari hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, aliwataka watumishi wa afya kuwa wabunifu katika utendaji kazi wao ili kuboresha huduma. Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kujifunza, kuboresha ujuzi na kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi huku akiwapongeza kwa juhudi zao za kutoa huduma bora katika eneo hilo, na kuwataka kuwa mfano wa uzalendo na utumishi bora kwa jamii.

Nae Rais wa Chama cha Wataalamu wa Masiko, Koo na Pua, Dk. Edwin Liyombo, alisema lengo la uwepo wa siku ya usikivu duniani ni kuhamasisha wananchi, wataalamu wa afya na watunga sera kulipa kipaumbele tatizo la usikivu kwa kuonyesha athari wanazoweza kupata watu wasipopata huduma ya afya ya masikio na usikivu. Madaktari hao wameweka kambi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kwa ajili ya kutoa elimu na huduma za uchunguzi wa awali wa masiko na usikivu bila malipo katika maadhimisho ya wiki ya usikivu duniani yanayofanyika kitaifa hospitalini hapo na kilele chake ni leo.



Mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya wahudumu wa kwenye mabasi ya masafa marefu yaliyoandaliwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) akikabidhiwa cheti cha kuhitimu mafunzo hayo na Mkuu wa Kituo cha Umahiri katika Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji cha NIT, Dk. Chacha Ryoba, mwishoni mwa wiki, kulia ni Ofisa Mfawidhi wa LATRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Shabani Mtende. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahudumu wa mabasi walia usumbufu vyombo vya dola

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHUDUMU wa kwenye mabasi ya masafa marefu nchini wamewalalamikia maofisa wa serikali na vyombo vya dola wanaosimamisha mabasi bila sababu kuwa wanasababisha usumbufu kwao na kwa abiria.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya walipokuwa wanahitimu mafunzo ya siku tano ya sheria za usafirishaji yaliyoandaliwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (LATRA).

Sophia Laiser ambaye alisoma risala ya wahitimu hao, alisema wamekuwa wakikumbana na vikwazo mbalimbali kutoka kwa maofisa wa serikali wanaposafiri na mabasi hali ambayo inasababisha huduma kwa wateja wao kutokuwa nzuri.

Alisema wakati mwingine mabasi yao yanakuwa yamekidhi vigezo vyote na hayana upungufu lakini maofisa wa serikali wanawasimamisha muda mrefu bila sababu.

"Tunaomba serikali na mamlaka zote zinazohusika kwenye hii sekta yetu ya usafirishaji zitusaidie kupunguza vikwazo hivi ili tuendelee kutoa huduma bora kwa wateja wetu," alisema Sophia.

Naye Neema Mwakatali alisema wamekuwa wakikabiliana na vikwazo hivyo kwa kutumia njia ambazo siyo sahihi ikiwamo kushuka kwenye basi na kwenda kuzungumza na maofisa hao jambo ambalo kupitia mafunzo waliyoyapata hawatakiwi kufanya.

Alisema kwenye mafunzo hayo walielekezwa na wakufunzi kwamba askari ama ofisa yeyote anayesimamisha basi kwenye eneo lolote anatakiwa kuingia kwenye basi na kuyaeleza matatizo aliyoyabaini huku abiria wakisikia.

"Tunashukuru mafunzo haya yametusaidia kutufungua macho, tumekuwa tukisimamishwa katikati ya safari na wakati mwingine unakuta basi halina shida yoyote lakini tunasimama muda mrefu, lakini kuna vitu ambavyo huwa vinafanyika ambavyo siwezi kuvieleza kwa sababu ni kinyume cha sheria," alisema Neema.

Mkuu wa Kituo cha Umahiri katika Taaluma za Anga na Oparesheni za Usafirishaji wa NIT, Dk. Chacha Rioba, alisema chuo hicho kwa kushirikiana na LATRA waliamua kutoa mafunzo hayo kwa wahudumu wa kwenye mabasi kutokana na sekta hiyo kukabiliwa na ufanisi mdogo.

Alisema wahudumu hao wa kwenye mabasi wamekuwa wakifanya kazi hiyo bila kuwa na uelewa mzuri sheria za usafirishaji hali ambayo ilikuwa inasababisha matatizo.

Alisema mafunzo hayo yanafadhiliwa na serikali kupitia mradi wa ISTRIP ambao uko chini Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwamba mafunzo hayo yamekuwa yakiwahusisha pia madereva wakiwamo wa magari ya serikali.

"Mpaka sasa tumeshatoa mafunzo haya kwa madereva 614 na hawa wahudumu tumewafikia zaidi ya 150 kwenye kanda zote ambazo tumefika, lengo la mafunzo ni kuboresha sekta hii ya usafirishaji, imebainika kuwa wahudumu wamekuwa wakikwaruzana na mamlaka kutokana na kutojua sheria," alisema Dk. Ryoba.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Shabani Mtende, alisema lengo la mamlaka hiyo ni kuirasimisha sekta ya wahudumu wa kwenye mabasi ili kuongeza ufanisi zaidi.

Alisema wahitimu wa mafunzo hayo watakuwa wanasajiliwa na kupatiwa vitambulisho maalumu ambavyo watatakiwa kuwa navyo wakati wote wa kutekeleza majukumu yao na kwamba itafika muda muhudumu ambaye hajapata mafunzo hayo hataruhusiwa kufanya kazi.

# H'shauri yagawa taulo za kike kwa wanafunzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI wa kike 8,552 wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Mji Njombe, wamepatiwa taulo za kike zenye thamani ya Sh. milioni 15 ili kupunguza utoro na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa taulo hizo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe, Erasto Mpete, aliwahimiza walimu kuhakikisha taulo hizo zinawafikia walengwa na sio vinginevyo.

"Halmashauri ya Mji Njombe inatambua umuhimu wa kuwasaidia wanafunzi wa kike ndio maana Baraza la Madiwani waliamua kutenga Sh. milioni 15," alisema Mpete.

Mpete alisema kuwa lengo la kugawa taulo hizo ni kuwasaidia wanafunzi wa kike wasipate changamoto wakiwa kwenye masomo yao na kupunguza utoro shuleni.

"Baadhi ya wanafunzi wa kike walikuwa wakikosa masomo kwa sababu ya kukosa vifaa vya kujisitiri hivyo hii ikawe njia ya kumwinua kitaaluma mtoto wa kike awapo shuleni," alisema Mpete.

Hata hivyo Mpete alitoa rai kwa wanafunzi kwa kuzingatia nidhamu kwa walimu, wazazi na walezi na kukemea wanafunzi kujihusha na mahusiano katika umri mdogo jambo ambalo limekuwa likichangia kuharibu maadili.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Thadei Luoga, alisema taulo hizo zitaenda kuimarisha usafi kwa watoto, usawa kwa watoto wa kike kupata elimu pia kuongeza ufaulu kwa watoto wa kike.

"Tangu ugawaji huu umeanza umesaidia pia mtoto wa kike wa Halmashauri ya Mji Njombe kujiamini awapo katika siku zake," alisema Luoga.

Kwa upande wao wanafunzi akiwemo Lucia Mgaya alisema tangu wameanza kugawiwa taulo za kike hata utoro kwa wanafunzi wa kike umepungua.

"Kwanza tulikuwa hatujiamini kwa sababu wakati mwengine hedhi inakukuta ukiwa haujajiandaa na nyumbani fedha za kununulia pedi hakuna sasa unalazimika kutoroka ili ubaki nyumbani," alisema Mgaya.

Agnes Sanga alisema njia ya kitambaa waliyokuwa wakitumia hapo mwanzo kujisitiri haikuwa salama kwa sababu ilikuwa ikiwasababishia magonjwa ya kuwashwa mara kwa mara.

Alisema anaishukuru Halmashauri ya Mji Njombe kwa kuwapa taulo hizo kwa sababu zinawafanya kuudhuria masomo kwa wakati pamoja na kuwa wasafi muda wote.



## Ujenzi wa barabara Chakechake waongezwa muda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, amesema ujenzi wa barabara ya Chakechake hadi Wete Pemba umeongezewa muda hadi Januari 2025, kutokana na changamoto zilizojitokeza

Alisema ujenzi huo ulianza rasmi Februari, 2022 na ulitegemewa kukamilika Agosti, 2024 lakini ulikumbana na changomoto mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa kazi, kulikotokana na kubadilika kwa mpango wa ujenzi.

Aliyasema mwishoni mwa wiki akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe, katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani nje kidogo ya Mji wa Zanzibar.

Alisema kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Chake -Wete, ujenzi wake bado uko ndani ya muda na haujachelewa kama inavyodaiwa.

Hivyo, alisema serikali inamtaka mkandarasi huyo ambaye ni Kampuni ya MECCO imalize kazi ya ujenzi wa Barabara ya Chake - Wete yenye urefu wa kilomita 22 kwa muda uliopangwa.

"Barabara hii kwa mujibu wa mkataba ni kufanyiwa matengenezo makubwa (Rehabilitation) lakini kilichofanyika ni kujengwa upya na kuchelewa kwa ulipaji wa fidia za majengo." Alisema Dk. Khalid.

Aidha alisema mkandarasi alianza na zana chache kulingana na mahitaji ya awali ya ujenzi na aliendelea kuongeza zana siku hadi siku kulingana na kazi zinavyoongezeka.

# Rais Samia aongoza Watanzania kumwombea Hayati Ali Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan jana amewaongoza wananchi mbalimbali katika dua maalum (hitma) ya kumwombea Rais mstaafu wa awamu ya pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi katika viwanja vya Nyamanzi nje ya mji wa Zanzibar.

Dua hiyo iliyoandaliwa na Rais Samia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kiserikali akiwamo Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, viongozi wa dini wakiwamo kutoka Lamu nchini Nairobi, viongozi wa kisiasa na wananchi mbalimbali.

Akizungumza baada ya dua hiyo, Rais wa Zanzibar Dk. Mwinyi alitoa siri ya sababu ya Mzee Mwinyi wakati akiuguwa kulia sana alipotembelewa na Rais Samia akiwa nyumbani kwake Mikocheni jijini Dar es salaam.

Dk. Mwinyi alisema mzee wake huyo alilia kwa furaha kutokana na mchango mkubwa alioutoa Rais Samia katika kumhudumia kupata matibabu ndani na nje ya nchi. "Natoa shukurani zangu kwa dhati kwa Rais Samia ametufanyia wema mkubwa mno tangu mzee wetu ameanza kuugua mwezi Novemba, amepelekwa Uingereza kwa matibabu tupo nae, anatuuliza hatua kwa hatua, anapewa taarifa na vyombo vya serikali na anatuliwaza," alisema.

Dk. Mwinyi alisema Rais Samia alihakikisha kilichohitajika wakati wa matibabu ya baba yake kinapatikana mpaka madaktari waliporuhusu mgonjwa arudi nyumbani na hakuacha kumtembelea. "Aliyosema ndugu yangu Abdallah jana pale viwanja vya Amani wakati wa kuaga mwili wa marehemu, na mimi shahidi nilikuwapo ziara ya mwisho ya Rais Samia kuja kumtembelea mzee wetu nyumbani kwake kweli alilia, na alilia kwa furaha ya kumwona rais wetu, alilia kwa wema aliomfanyiwa na rais wetu," alisema.

Dk. Mwinyi pia aliwashukuru madaktari na wauguzi katika Hospitali ya Mzena alipokuwa akitibiwa baba yake kwa kuwa muda wote walikuwa karibu naye kumpatia huduma na msaada aliohitaji.

Hata hivyo alisema amepokea ombi la Rais Samia kuwa mbuyu wa familia ya Mzee Mwinyi ingawa sio rahisi kuwa kama baba yake ingawa alimpa wosia kuwa msimamizi wa familia.

"Mzee alituita siku moja akatuambia nyinyi vijana wangu siku zilizobaki za kuishi sio nyingi kwa hivyo nakuombeni muunge udugu na akanitaja mimi kwa jina Hussein nakuagiza kuwa wewe utakua msimamizi wa familia.

Sio kwa sababu wewe ni mkubwa, wapo wakubwa zako lakini kutokana na wadhifa uliokuwa nao waweke ndugu zako hawa chini ya mwongozo wako, nikalipokea namuomba Mwenyezi Mungu anisaidia," alisema.

Dk. Mwinyi pia alitoa shukrani kwa mashehe na walimu kwa dua nyingi walizomwombea mzee wao na kumhifadhi katika nyumba yake ya milele.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na familia ya Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, alipokwenda kuhani msiba kufuatia kifo cha Mzee Masauni Yussuf Masauni aliyefariki dunia Februari 23, mwaka huu. Rais Samia amekutana na familia hiyo nyumbani kwao Migombani, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwalimu Nyerere, wadau wajadili kozi ya jamii ngazi ya shahada

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHUO cha Mwalimu Nyerere kimekutana na wadau kujadili mtaala wa mwendelezo wa jamii kwa ngazi ya shahada na shahada ya uzamili.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao hicho kilichofanyika Chuo cha Mwalimu Nyerere Visiwani Zanzibar Mkuu wa Fedha na Utawala chuoni hapo, Dk. Mery Kirupi, alisema kikao hicho ni sehemu ya maandalizi ya mtaala ili chuo hicho kianze kutoa kozi hiyo.

Alisema kwa sasa wana mitaala kwa ngazi ya cheti na shahada hivyo wahitimu chuoni hapo wanakosa mwendelezo wa ngazi hiyo kutokana na mahitaji ya wanajamii. "Mtaala tunaouandaa ni maendeleo ya jamii kwa ngazi ya shahada na shahada ya uzamili na tumeamua kufanya hivyo kutokana na wanafunzi na wanajamii wanahitaji kuwa na kozi ya maendeleo ya jamii," alisema.

Alisema baada ya kuandaa mjadala huo watauwasilisha katika bodi za usimamizi na watakapouona unafaa wataanzisha kozi hiyo kwa ngazi hiyo na wanataka mani kuanza kutoa mwakani kutokana na uhitaji wa jamii.

Alisema michango iliyotolewa na wadau wa kikao hicho ni mizuri na inajenga na itasaidia kuweka mtaala kuwa mzuri na kunza kutoka kozi ya ngazi hiyo wahitimu watakuwa na ubora wa maendeleo ya jamii.

Aidha alisema moja ya changamoto inayowakabili wanafunzi wa vyuo hasa wanapoenda katika kazi za vitendo katika ofisi mbalimbali hukabiliana na changamoto za udhalilishaji.

Alisema baadhi ya wasimamizi wa wanafunzi hao hutaka wapewe malipo jambo ambalo sio sahihi na wanapaswa kufanya majukumu yao kuwasimamia ili kupata uzoefu.

Aliwataka wanafunzi wanaokumbana na changamoto hiyo kuripoti sehemu husika huku wakiwa na vielelezo ili watuhumiwa wa makosa hao kuchukuliwa hatua za haraka.

Naye Dk. Sara Mwakambiki Mkuu wa Idara ya Stadi ya Jinsia chuoni hapo alisema chuo kipo katika mkakati wa kuinua hali ya uwepo wa mitaala mbalimbali.

Kuhusu changamoto ya udhalilishaji kwa wanafunzi wanapokwenda katika ofisi mbalimbali kusoma kwa vitendo, kabla ya kuondoka hupewa elimu ya kujitambua ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Alisema kati ya mwnafunzi mmoja kati ya wanne duniani, hukutana na changamoto hiyo ya udhalilishaji na chuoni hapo kuna dawati la jinsia ili kuwasilisha changamoto hizo na kufanyiwa kazi. "Tunawawezesha wanafunzi kuwapa elimu ya kujitambua, kuongea na kutetea haki zao ingawa changamoto hiyo sio kubwa sana chuoni hapa lakini ipo ulimwenguni," alisema.

# Watoa vifaa vya kujifungulia kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi

**Na Boniface Gideon,** MUHEZA

VIFO vya watoto wachanga vimeshuka kutoka 556 kati ya vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo 104 kwa vizazi hai 100,000 nchini kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali.

Hatua hizo zinajumuisha ujenzi wa vituo vipya vya kutolea huduma za afya katika maeneo ambayo hayakuwa navyo na kutoa elimu kuhakikisha wajawazito wanajifungulia katika vituo vya afya badala ya nyumbani.

Katika kuunga mkono mikakati ya serikali kukabiliana na vifo vitokanavyo na uzazi, Shirika lisilo la kiserikali la Muheza Kwanza limetoa msaada wa vifaa vya kujifungulia kwa kinamama zaidi ya 200 katika Vituo vya Afya Mkuzi na Ubwari, vyote wilayani Muheza.

Msaada huo ni sehemu ya mpangokazi wa shirika hilo wa kuisaidia jamii katika sekta za afya, elimu, maji na uwezeshaji wa kijamii.

Akikabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Muheza kwanza, Hamis Rajabu, alisema shirika hilo linaundwa na wazaliwa wa Muheza wanaoishi nje ya wilaya hiyo.

"Sisi ni wazaliwa wa Muheza tunaoishi nje ya wilaya yetu na wengine wako nje ya nchi. Tumejiunda na kuwa shirika kwa lengo la kuibadilisha kimaendeleo wilaya yetu.

"Tumeunda shirika letu la Muheza Kwanza kwa ajili ya kuisaidia serikali kutatua changamoto zinazokabili wananchi wa Muheza," alisema.

Kiongozi huyo alisema vifaa vya kujifungulia walivyokabidhi, vitawezesha kinamama zaidi ya 200 kupata huduma ya kujifungua bila changamoto kubwa.

"Sote tunafahamu kuwa serikali yetu inapambana kuboresha huduma za afya hususani afya ya mama na mtoto. Kupitia vifaa hivi, tunaamini tutasaidia kuongezea palipopungua na kuwawezesha kinamama kujifungua salama kabisa," alisema.

Rajabu alisema wataendelea kusaidia kuboresha huduma za afya, elimu, maji na uwezeshaji wa kijamii.

"Huu ni mwanzo tu wa mpangokazi wetu kwa Wilaya yetu ya Muheza. Tuna mambo mengi ya kufanya hususani kwenye sekta za afya, elimu na maji pamoja na uwezeshaji wa kijamii.

"Tutaendelea kushirikiana na serikali yetu katika kupunguza changamoto kubwa zinazowakabili wananchi wa Muheza," alisema.

Akipokea msaada huo, Ofisa Utawala Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Nelson Kasiki, alishukuru shirika hilo kwa msaada huo unaolenga kusaidia kuboresha huduma za uzazi.

"Niwashukuru sana Muheza Kwanza kwa msaada huu ambao unakwenda kusaidia kinamama kujifungua salama.

"Pia niwapongeze kwa kuungana na kutengeneza shirika ili kusaidia wananchi wa Muheza. Ni jambo zuri na la kuigwa.

"Niwaombe wadau wengine nao wajitokeze kusaidia zaidi ya hapa. Bado jamii yetu ina uhitaji mkubwa wa huduma muhimu za kibinadamu," alisema Kasiki.

Pia alielekeza watoa huduma za afya kufanya kazi kwa weledi kwa kufuata miongozo ya afya na kujiepusha na tabia zinazochafua sifa ya huduma za afya.

"Kwa siku za hivi karibuni tumekuwa tukisikia taarifa kupitia vyombo vya habari wahudumu wa afya kukengeuka, niwaombe wahudumu wa afya acheni kutoa lugha chafu kwa kinamama hususani wajawazito, pia vifaa hivi vikatumike kama watoaji walivyolenga, msije mkaenda kuviuza," aliagiza.




Ofisa Utawala Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Nelson Kasiki (kulia), akipokea vifaa vya kujifungulia wajawazito vilivyotolewa na Shirika la Muheza Kwanza mjini Muheza mwishoni mwa wiki. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Korti kupokea taarifa ya uuzwaji nyumba ya mtoto wa Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi leo inatarajia kupata taarifa ya utekelezaji amri iliyotoa ya kukamata nyumba ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe kwa kushindwa kulipa Sh. milioni 62.7 za malimbikizo ya mishahara ya waandishi wa habari 10 wa gazeti hilo.

Shauri hilo lilipangwa kutajwa leo na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio Februari 13, mwaka huu baada ya kukubali maombi ya wadai na kumteua dalali wa kukamata nyumba kwa ajili ya kuipiga mnada.

Februari 28 mwaka huu, Dalali wa Mahakama, Jesca Massawe alifanikiwa kubandika matangazo ya kukamata nyumba ya mkurugenzi huyo tayari kupigwa mnada kufidia deni la malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi.

Dalali Jesca alifika nyumbani kwa Mkurugenzi Dudley saa tatu asubuhi siku hiyo, Dudley alitoka nje akamwambia jukumu lililompeleka hapo kisha akaanza kubandika matangazo ya kukamata nyumba kwa agizo la Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi.

Mkurugenzi Dudley hakuridhishwa na utaratibu huo, hivyo aliomba matangazo yasibandikwe, Dalali Jesca alikataa na kuamua kubandika matangazo hayo nje ya nyumba, kwenye geti la kuingia ndani na mengine akabandika ukutani nje ya nyumba hiyo.

Dudley aliamua kuyabandua matangazo yote licha ya kupewa angalizo la kutoyaondoa kwa kuwa ni maagizo ya Mahakama Kuu.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio alitoa amri hiyo baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume la Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Julai 2023.

Katika shauri hilo namba 28461 la mwaka 2023, wadai ni Maregesi Paul na wenzake tisa dhidi ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe.

# Mvua ya mawe yaangusha nyumba 70, kuku 300 wafa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MVUA ya mawe iliyoambatana na upepo mkali, imeangusha nyumba 70 katika Kata ya Kizumbi Manispaa ya Shinyanga, ikiua kuku 300 na kusababisha makumi ya wananchi kukosa makazi huku wengine wakijeruhiwa.

Ni tukio la usiku wa kuamkia jana, mvua hiyo iliponyesha saa tano usiku na kuezua nyumba, 70 zimeathiriwa zaidi.

Akisimulia tukio hilo, Diwani wa Kizumbi, Rubeni Kitinya alisema katika Kijiji cha Bujinge, zimeanguka nyumba 20 ambako kaya 11 hazina makazi kabisa na Kijiji cha Bugayambelele zimeanguka nyumba 50 na kaya nane hazina makazi. Wakazi wake wamepewa hifadhi shuleni.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Bugayambelele, Emmanuel Wiliamu, alisema kuwa wakati mvua inanyesha, ghafla walianza kusikia mawe na upepo mkali; ndani ya dakika tano nyumba zilianza kuanguka huku wananchi wakikimbilia nje ili kunusuru maisha yao.

Mmoja wa wananchi walioathiriwa, Mzee John Kashinje, alisema wakati mvua inanyesha, akiwa amelala alishangaa nyumba inaporomoka, ndipo ikapinda kichwa akielekeze ukutani, huku mwili wote ukifunikwa na matofali, mbinu hiyo anaitaja "ndiyo salama yangu".

Mwananchi mwingine Nkwangu Shija, alisema wakati nyumba ilipoanza kuanguka walikimbilia nje, lakini bahati mbaya mtoto wake, Retisia Shija (4) alifikiwa na tofali la ukuta ulioanguka, likimjeruhi kichwani. Sasa anaendelea kupatiwa matibabu hospitalini.

Mfugaji wa kuku, Neema Lock, alisema wakati mvua hiyo inanyesha, iliezua mabanda ya kuku na ukuta kuangukia baadhi ya kuku na kusababisha kuku wake 300 kufa.

Mratibu wa Maafa Manispaa ya Shinyanga, Revocutus Rutunda, aliyefika katika eneo hilo la tukio, alisema wanaendelea na tathmini ili kupata idadi kamili ya wananchi ambao wameathiriwa na mvua hiyo.

Alisema kwa waliokosa hawana makazi kabisa, tayari wameshawatafutia maeneo ya shule kwenda kupata hifadhi ya muda, huku watu wawili ambao wamepata madhara makubwa baada ya kupondwa na nyumba wakipelekwa hospitalini kupata matibabu.

HABARI KIMATAIFA

# Wapalestina wengine 90 wafariki Rafah

**GAZA,** Palestina

WAKATI mazungumzo ya usitishaji vita yakianza tena kati ya Israel na Hamas huko Cairo nchini Misri, Wizara ya Afya imebainisha kuwa watu 90 wamefariki ndani ya saa 24 zilizopita wakiwamo 14 wa familia moja katika shambulizi la anga lililofanya na Israel huko Rafah.

Wizara hiyo ambayo iko chini ya Hamas inasema takriban miezi mitano ya operesheni za kijeshi za Israel zilizoanzishwa kulipiza kisasi shambulio la Hamas nchini Israel Oktoba 7, 2023 hadi sasa zimesababisha vifo vya watu 30,410 katika Ukanda wa Gaza, wengi wao wakiwa ni raia.

Inaelezwa kuwa mashambulizi mengine kadhaa ya anga yalilenga miji ya Khan Younes na Rafah kusini wakati wa usiku, huku serikali ya Hamas ikisema moto mkubwa wa mizinga ulilenga Jabaliya, Beit Hanoun, Zeitoun na Tal al-Hawa kaskazini.

Katika hatua nyingine Marekani inasema mazungumzo hayo kati ya mahasimu hao wawili yanaendelea huko Misri ili kufikia mwafaka wa Gaza na makubaliano ya kuwaachilia mateka.

Wakati mazungumzo hayo yakiendelea kundi la wanamgambo la Hamas linasema makubaliano ya kusitisha mapigano yanaweza kutiwa saini ndani ya saa 24, hadi 48 ikiwa Israel itakubali matakwa yake.

Inaelezwa kuwa suala hilo linasalia kuwa suluhu ya kubadilishana mateka na wafungwa wa Kipalestina kwa ajili ya mwezi mtukufu wa Ramadhan ambao utaanza baada ya wiki moja.

Pia inaelezwa kuwa maofisa wa Israel wanasubiri majibu ya Hamas kwa mfumo elekezi ulioanzishwa katika mkutano wa Paris. Katika hatua ambayo Israel inasitisha ushiriki wake katika mazungumzo yanayoendelea Cairo na kuitaka Hamas kwanza itoe orodha ya mateka inayowashikilia huko Gaza na ambao bado wako hai.

Aidha, inaelezwa kuwa hakuna jibu la moja kwa moja kwamba Israel imekubali pendekezo la kusitisha mapigano, kutokana na maneno yaliyotumiwa na ofisa mkuu wa Marekani.

Licha ya hayo inaelezwa kuwa kwenye meza ya mazungumzo kuna suluhu ya wiki sita na pia kuachiliwa kwa mateka wanaochukuliwa kuwa walio hatarini zaidi, wagonjwa, waliojeruhiwa, wazee na wanawake. Huo ukiwa ni mtazamo wa Waisraeli jambo ambalo bado linasubiriwa kupatiwa muafaka.

Ofisa Mkuu wa Palestina ambaye hakutaka jina lake litajwe anasema "ikiwa Israel itakubali matakwa ya Hamas, ambayo ni pamoja na kuwarejesha Wapalestina waliokimbia makazi yao kaskazini mwa Gaza na kuongezeka kwa misaada ya kibinadamu, hii inaweza kufungua njia ya makubaliano ya mapatano ndani ya saa 24 au 48 zijazo."

Msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) Jens Laerke, anasema mgogoro huo wa Israel na Hamas umesababisha maafa ya kibinadamu na njaa isiyoepukika kwa watu milioni 2.2, wengi wao wakiwa ni wakazi wa Gaza.

**FEDHA YAGEUKA KINGA**

Kutokana na zoezi la kuondoka Gaza ili kulinda usalama kuwa gumu kwa miongoni mwa raia wengi wa eneo hilo, inabainishwa kuwa kwa sasa wanalazimika kulipa fedha ili kuondoshwa katika eneo hilo.

Taarifa zinaeleza kuwa kuondoka katika eneo hilo kwa uhakika kunahitaji watu walipe maelfu ya dola na ili kuingiza majina yao kwenye orodha ya watu walioidhinishwa kuondoka kupitia kivuko cha Rafah kwenda Misri.

Inaelezwa kuwa kivuko hicho kimefungwa kwa idadi kubwa ya watu chini ya kizuizi cha Misri na Israel dhidi ya Hamas.

Taarifa zinasema ni baadhi tu ya wamiliki wa pasipoti za kigeni na wategemezi wao wameweza kuondoka, pamoja na baadhi ya watu waliojeruhiwa vibaya na wagonjwa na wale wanaoandamana nao.

Hata hivyo, kuna mfumo sambamba ambao wananchi wa Gaza wanalipa madalali wa Misri kuingia kwenye orodha ya watu wanaoweza kuondoka.

Bei inaelezwa kuwa huanzia dola 6,000 (Sh. milioni 15.2) kwa kila mtu hadi zaidi ya dola 12,000, (Sh. milioni 30.5) kiasi kinachotajwa kuwa kikubwa mno kwa wakazi wengi wa Gaza.

Vile vile, inaelezwa kuwa bado idadi inayoongezeka ya watu waonajaribu kutafuta pesa ili kukimbia, kwa msaada wa marafiki na familia huko Amerika na Ulaya. **RFI, BBC**

## Wanajeshi wawili wa Afrika Kusini wafariki DRC

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

JESHI la Afrika Kusini limesema wanajeshi wake wengine wawili wameuawa wakiwa wanalinda amani huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, (DRC), huku ikidaiwa kuwa sababu ya vifo hivyo ni ugomvi wa wenyewe kwa wenyewe.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na jeshi hilo na kunukuliwa na shirika la habari la AFP, tukio hilo limetokea juzi baada ya mmoja wa wanajeshi hao kumshambulia mwenzake na kumpiga risasi, kabla ya kujipiga risasi mwenyewe.

Taarifa hiyo inasema kuwa maofisa hao wamekufa wakiwa sehemu ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa wa (MONUSCO), ambao tayari wameanza kuondoka nchini humo.

Pia inaelezwa kuwa takriban wanajeshi 2,900 kutoka Afrika Kusini wanashika doria DRC, kama sehemu ya kikosi cha (SADC) kilichotumwa na serikali kukabiliana na waasi wa M23.

Wanajeshi wengine wawili wa Afrika Kusini waliuawa mwezi uliopita kupitia shambulizi la kombora, tukio lililosababisha vyama vya upinzani vya Afrika Kusini kudai kwamba walitumwa DRC bila kuwapo kwa mipango ya kutosha ya kiufundi. **VOA**



Wananchi wa Palestina wakitembea katikati ya magofu na vifusi vya makazi yao yaliyoharibiwa na mashambulizi ya Israel. **PICHA: MTANDAO**

## Kiongozi wa kijeshi Chad kuwania urais

**N'DJAMENA,** Chad

KIONGOZI Mkuu wa utawala wa kijeshi nchini Chad, Mahamat Itno, amesema kuwa atawania uchaguzi wa urais wa Mei 6, mwaka huu ikiwa ni siku tatu tu baada ya mpinzani wake mkuu kuuawa katika mazingira ya kutatanisha.

Aliyabainisha hayo jana, Itno ambaye inaelezwa kuwa alichukuwa madaraka mwaka 2021 baada ya baba yake, kiongozi mkongwe Idriss Itno, kufariki wakati akipambana na waasi.

Kiongozi huyo aliyetawala kwa mkono wa chuma alikuwa ameiongoza nchi hiyo kwa zaidi ya miongo mitatu. Na kwamba alitangazwa kuwa rais wa mpito na uongozi wa kijeshi na aliahidi kurejesha utawala wa kiraia na uchaguzi katika kipindi cha miezi 18.

Inaelezwa kuwa kuongozi huyo wa kijeshi aliendia tofauti na ahadi yake kwa kuongoza kipindi cha mpito kwa miaka miwili. Huku akitangaza kuwania urais miezi miwili kabla ya kupiga kura.

Itno mwenye umri wa miaka 39 ana uhakika wa kushinda kutokana na mpinzani wake mkuu Yaya Djeru kuuawa Jumatano na upinzani kukandamizwa. **DW**

HABARI MICHEZO

# MASHUJAA FC YAANZA KUJIONDOA HATARINI, WAZIRI PIGA BAO LA SABA

Na Adam Fungamwango

HATIMAYE Timu ya Mashujaa FC imeanza kujiondoa taratibu kwenye mstari wa kushuka daraja baada ya juzi kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo FC, mechi ikichezwa Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

**Bao pekee la Adam Adam, limeifanya timu hiyo kutoka kwenye nafasi ya 15 iliyokuwa inaishikilia kwa muda mrefu na sasa imepanda hadi ya 13, ikifikisha pointi 18.**

Timu hiyo imeziacha chini Mtibwa Sugar inayoburuza mkia na pointi 12, Geita Gold nafasi ya 15 ikiwa na pointi 18 na Tabora United nafasi ya 14, ikiwa pia na pointi 18.

Mashujaa inakaa juu ya timu hizo kutokana na kuwa na idadi kubwa ya mabao yakufunga, ikipachika 17 ambayo ni mengi kuliko timu zilizopo nyuma yake.

Kipigo hicho kinaifanya Namungo kubaki nafasi ya tisa, ikiwa na pointi 29, ikipoteza mechi ya sita msimu huu.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu iliyochezwa juzi, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, ilishuhudia KMC ikilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold.

Yusuph Mhilu alianza kuiandikia Geita Gold bao dakika ya 45, kabla ya Waziri Junior kusawazisha dakika ya 56, likiwa ni bao lake la saba kwenye Ligi Kuu msimu huu.

KMC bado imeng'ang'ania kwenye nafasi ya tano, ikifikisha pointi 25, huku Geita Gold ikiwa nafasi ya 15. Mechi nyingine ilipigwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, wakati wenyeji Kagera Sugar walipolazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania.

Edward Songo aliwafungia wageni bao dakika ya 22, kabla ya Mubarack Amza kusawazisha kwa penalti dakika ya 41.

Ni matokeo yanayoipeleka Kagera Sugar kwenye nafasi ya saba ikiwa na pointi 23, JKT Tanzania ikiwa nafasi ya 12 na pointi zake 19.



TUMEWAKANDA...




Wachezaji wa Simba wakifurahia baada ya kumalizika kwa mchezo wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika na kushinda kwa mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Dar City yaanza BDL kwa kichapo*

Na Oliver Albert

BINGWA mtetezi wa Ligi ya Mpira wa Kikapu Mkoa wa Dar es Salaam (BDL), Dar City, imeanza vibaya ligi ya msimu huu baada ya juzi kupokea kipigo cha pointi 77-66 kutoka kwa JKT.

JKT ni kama wamelipa kisasi cha msimu uliopita baada ya kupoteza michezo mitatu kati ya minne waliyokutana na Dar City ambayo ilitwaa ubingwa.

Katika mchezo huo uliofanyika juzi usiku, timu zote zilianza mchezo kwa kasi na kujikuta zikimaliza robo ya kwanza zikiwa zimefungana pointi 21-21.

Robo ya pili JKT ilirudi kwa nguvu zaidi na kufanikiwa kwenda mapumziko ikiongoza kwa pointi 39-31.

Timu hizo ziliendelea kupelekeana 'moto' kwa kasi, lakini ni JKT waliokuwa wa moto zaidi wakionekana wamepania kulipa kisasi na hivyo kuongoza pia robo ya tatu kwa pointi 55-50.

Kocha wa JKT, Christian Jacob 'Webber', alisema amefurahi kuanza ligi vizuri kwa ushindi akiamini huo ni mwanzo wa kufanya vizuri zaidi msimu huu.

"Kushinda tena dhidi ya timu ngumu kama Dar City ni jambo la kushukuru na kwa kweli tumefurahi. Naamini ushindi huu utatupa morali kubwa katika michezo yetu ijayo kwa sababu msimu huu tumedhamiria kurudisha heshima kwenye BDL," alisema Christian.

Mechi nyingine kwa wanaume DB Oratory iliifunga Srelio pointi 80-59 wakati kwa upande wa wanawake mabingwa watetezi, Vijana Queens, walianza vizuri ligi kwa kuichapa City Queens pointi 90-25.

Jeshi Stars waliwafunga ndugu zao Twalipo Queens kwa pointi 95-23 kama ilivyo kwa JKT Stars waliposhinda kwa pointi 52-21 dhidi ya Mgulani Stars.

# FA Cup 36 bora Z'bar kuanza Alhamisi wiki hii

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HATUA ya 36 bora ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, itaanza kutimua vumbi Alhamisi hadi Jumapili wiki hii.

Awali, michuano hiyo ilipangwa kuchezwa leo Jumatatu, lakini ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar ikaahirishwa baada ya kusimama kwa ligi zote kwa ajili ya maombolezo ya kifo cha Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ), ligi zote zimeruhusiwa kuendelea kuanzia keshokutwa leo Jumatatu.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ZFF, ambao ndio waratibu wa michuano hiyo, Ali Bakar, alisema maandalizi ya kuelekea michuano hiyo kwa timu zilizotinga hatua ya 36 bora tayari yamekamilika.

Alisema klabu zote zimeshapewa ratiba hiyo ambayo imefanyiwa marekebisho ambapo michuano hiyo itachezwa kabla ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuingia.

Alisema ratiba hiyo imezingatia mabadiliko ya ratiba ya Ligi Kuu ya Zanzibar ambayo nayo iteendelea kuanzia leo Jumatatu.

"Ratiba ya FA inatokana na nafasi tutakayopata katika ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar, hii ni kutokana na kuzipa nafasi klabu kumalizia michezo yao ya ligi kwa mzunguko husika," alisema.

Hata hivyo, azitaka klabu zote kuzingatia ratiba mpya iliyotolewa pamoja na kufanya maandalizi kuelekea michuano hiyo kwa hatua iliyopo.

**Ratiba ya FA inatokana na nafasi tutakayopata katika ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar, hii ni kutokana na kuzipa nafasi klabu kumalizia michezo yao ya ligi kwa mzunguko husika.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MUSIALA AIGOMEA BAYERN

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Jamal Musiala, amekataa mkataba mpya katika Klabu ya Bayern Munich, akilenga kuhamia Ligi Kuu England msimu wa majira ya joto, huku Manchester City na Liverpool wakiongoza katika kinyang'anyiro cha kumwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Star)***

### TUCHEL KUFUKUZWA MAPEMA

KOCHA Thomas Tuchel huenda akafutwa kazi ikiwa Bayern Munich itapoteza mchezo wao wa mkondo wa pili wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lazio Jumanne. ***(Sky Sports)***

### HAG AMFUATILIA GUTIERREZ

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anamfuatilia mlinzi wa Girona, Miguel Gutierrez mwenye umri wa miaka 22 kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Sun)***

### AMORIM ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imezidisha nia yao ya kutaka kumchukua Kocha Mkuu wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, lakini Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, anabakia kuwa mstari wa mbele kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp. ***(Mirror)***

### YAKOMALIWA ARSENAL

ARSENAL inamfuatilia mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 19, huku wakipania kuimarisha safu yao ya ushambuliaji msimu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### BARCA KUMKOSA ZEBRI

MATUMAINI ya Barcelona kumteua Kocha wa Brighton, Roberto de Zerbi, msimu wa majira ya joto yametatizwa na kukataa kwa Seagulls hao kufanya mazungumzo kuhusu kipengele cha kuachiwa cha euro milioni 15 cha Muitaliano huyo. ***(Sport)***

### FLICK ATAJWA BARCA

KLABU ya Barcelona imefanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Ujerumani, Hansi Flick, kuhusu kurithi mikoba ya Xavi. ***(Florian Plettenberg)***

### ZAHA AFUATILIWA EVERTON

KLABU za Fulham, Everton, West Ham na Wolves, zinamfuatilia winga wa Galatasaray mwenye umri wa miaka 31 raia wa Ivory Coast, Wilfried Zaha. ***(Ekrem Konur)***

### ARSENAL, CITY KWA KAYODE

ARSENAL na Manchester City zinashindana kumsajili mchezaji wa Fiorentina mwenye umri wa miaka 19 na beki wa pembeni wa Timu ya Taifa ya Italia chini ya umri wa miaka 21, Michael Kayode. ***(Fichajes)***

### RAPHINHA, KOUNDE KUUZWA

BARCELONA itaweka kipaumbele katika kuwauza winga wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 27 na mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde (25), msimu wa majira ya joto. ***(Sport)***

## DONDOO ...OKA MAGAZETI ...AYA



# MBAPPE, KOCHA PSG NI VITA CHINI KWA CHINI

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe alikutana na Kocha Luis Enrique, katika kituo cha mazoezi cha klabu hiyo ili kutatua mvutano unaotokana na kocha huyo wa Hispania kumbadilisha mchezaji huyo katika michezo ya hivi karibuni, kwa mujibu wa ESPN.

**Mbappe alitolewa nje baada ya kipindi cha kwanza katika suluhu dhidi ya Monaco, pia akitolewa baada ya dakika 65 za PSG katika sare na Rennes wiki moja kabla.**

Enrique alisema baada ya mechi ya Ijumaa kuwa ulikuwa uamuzi wake kumbadilisha nahodha huyo wa Ufaransa na nafasi yake kuchukuliwa na Randal Kolo Muani.

●●● Madrid yahusishwa na sababu kufanyiwa 'sab' mara kwa mara wenyewe wakutana...

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Mbappe mwenye umri wa miaka 25, hakufurahishwa na aliamua kumfuata kocha huyo ili kuzungumza naye suala hilo.

Na kocha huyo aliwaambia kwamba si jambo la kibinafsi na si kulipiza kisasi kwa uamuzi wa mshambuliaji huyo kuondoka PSG mwishoni mwa msimu huu.

Enrique alisema alimpigia simu kwani alihisi Mbappe hakuwa sawa kabisa na kumwambia hakukuwa na tofauti yoyote kati yao kabla ya kukutana juzi.

Kocha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania, aliongeza kuwa pia anafikiria kuhusu mustakabali wa timu hiyo, kama alivyowaambia waandishi wa habari kwamba wanatakiwa kujifunza kucheza bila Mbappe.

Lakini kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN, Mbappe anahisi mabadiliko hayo ni adhabu kwa uamuzi wake wa kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu.

Mbappe yupo kwenye mazungumzo na Real Madrid, ambao wana matumaini ya kumpata mshambuliaji huyo mwishoni mwa msimu huu.




# PULISIC SASA ATISHIWA KIFO

**MILAN,** Italia

WINGA wa AC Milan, Christian Pulisic, amepokea vitisho vya kuuawa na matusi kwenye mitandao ya kijamii baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Lazio kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Ijumaa.

Lazio ilimaliza mechi hiyo ikiwa na wachezaji nane huku Pulisic akiwa sababu katika kadi mbili nyekundu kati ya tatu zilizotolewa.

Pulisic alichapisha picha kwenye Instagram akiwa yeye na timu ya Milan wakishereheekea ushindi baada ya mchezo na alijikuta akiioga matusi kutoka kwa mashabiki wa Lazio ambao walimtishia kifo.

Pia kulikuwa na jumbe nyingi za kumuunga mkono Mmarekani huyo, zikiwamo kutoka kwa mchezaji mwenzake wa Milan, Theo Hernandez, ambaye aliandika, "Puliiiii mimi ni usalama wako."

Luca Pellegrini alitolewa kwa kadi nyekundu dakika ya 67 baada ya kadi mbili za njano zilizofuatana haraka - kila moja kwa kumchezea vibaya Pulisic.

Na Matteo Guendouzi alitolewa kwa kadi nyekundu dakika za lala salama kwa kujibu madhambi ya nyota huyo wa Marekani ambaye naye pia alilimwa kadi ya njano.

Beki wa Lazio, Adam Marusic alitolewa nje kwa kadi nyekundu dakika za lala salama.

Pulisic alijiunga na Milan akitokea Chelsea akitarajia kufufua maisha ya klabu hiyo.

Ana mabao saba na asisti sita katika mechi 25 za ligi hiyo hadi sasa.

# *Ancelotti alia na refa kuwanyima ushindi*

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema uamuzi wa mwamuzi "ambao haujawahi kushuhudiwa" uliona kile ambacho kingekuwa bao la ushindi la sekunde ya mwisho kutoka kwa Jude Bellingham kufutwa na kuwa katika sare ya 2-2 ya Real Madrid na Valencia Jumamosi.

Valencia waliongoza kwa 2-0 katika Uwanja wa Mestalla kwa mabao ya Hugo Duro na Roman Yaremchuk, kabla ya magoli mawili ya Vinicius Junior kusawazisha mambo kwenye uwanja huo ambapo alidhalilishwa kwa ubaguzi wa rangi na mashabiki msimu uliopita.

Bellingham alifikiri kuwa amechukua pointi zote tatu alipounganisha kwa kichwa krosi ya Brahim Diaz kwenye dakika ya tisa ya muda wa nyongeza, lakini mwamuzi, Jesus Gil Manzano aliamua kupuliza filimbi ya kumaliza mchezo mpira ukiwa hewani.

Kiungo huyo wa kati wa England alioneshwa kadi nyekundu kwa kupinga uamuzi huo, huku ripoti ya mwamuzi ikidai kuwa alionesha "mtazamo wa uchokozi" na mara kwa mara alipiga kelele.

"Hakuna mengi ya kusema. Kitu ambacho hakijawahi kutokea kilitokea," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tulimiliki mpira. Mchezo unapaswa kukoma wakati Valencia wanapokuwa na mpira. Haijawahi kutokea kwangu.

"Tulichukizwa na kadi nyekundu ya Bellingham. Hakutamka matusi yoyote. Alisema kwa Kiingereza 'ni goli', lakini alikuwa akisema tu kile ambacho sote tulikuwa tukifikiria. Nadhani mwamuzi alifanya makosa."

"(Bellingham) alikuwa wazi katika kile alichosema," aliongeza Ancelotti. "Alikuwa na hasira katika majibu yake, lakini hiyo ni kawaida, baada ya kile kilichotokea. Haikuwa tusi, hata kidogo."

Sare hiyo inawaacha Real Madrid kwa pointi saba kileleni mwa jedwali la LaLiga, huku wapinzani wao wa karibu Girona na Barcelona walikuwa uwanjani jana Jumapili.



# Mashabiki Chelsea wamchoka Pochettino

**LONDON,** England

SEHEMU kubwa ya mashabiki wa Chelsea walitoa hasira zao kwa wamiliki wa klabu hiyo, Waamerika na kocha Mauricio Pochettino juzi Jumamosi wakati 'The Blues' hao wakilazimishwa sare ya 2-2 na Brentford.

Washindi hao mara mbili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambao pia walishinda taji la Ligi Kuu England mara tano kati ya 2005 na 2017, wana msimu wa pili wa kukatisha tamaa, miaka miwili baada ya muungano unaoongozwa na Wamarekani kuchukua klabu hiyo na kuwekeza fedha nyingi kwa wachezaji.

Kutazama timu yao ikitupa uongozi wa 1-0 na kwenda 2-1 katikati ya kipindi cha pili ilikuwa ngumu sana kwa baadhi ya mashabiki wao kwenye Uwanja wa Gtech Community.

Kwanza zikaja kelele za "Roman Abramovich, Roman Abramovich" huku mashabiki wakitaka kutofautisha mafanikio yao chini ya mmiliki wa zamani wa klabu hiyo raia wa Urusi na nafasi yao ya katikati ya msimamo kwa sasa.

Kisha ukaja wimbo mkali kuhusu Todd Boehly, sura maarufu zaidi ya umiliki mpya wa Chelsea; huku wengine wakiinua picha ya kocha wa zamani Jose Mourinho, ambaye alishinda mataji matatu ya ligi hapo Stamford Bridge.

Na nyingine ikiwa ya Pochettino, kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur ambaye aliteuliwa kuwa kocha mkuu wa klabu hiyo ya Magharibi mwa London, Mei mwaka jana.

Mashabiki wengine wa Chelsea walitaka kukusanyika nyuma ya timu hiyo, ambayo hatimaye ilijizatiti na kupata sare ya mabao 2-2 wakati beki Axel Disasi alipofunga kwa kichwa dakika ya 83.

"Ni jambo la kawaida. Tulikuwa tukipoteza mchezo kwa mabao 2-1 na ni kuhusu kuonyesha kufadhaika," alisema Pochettino akiwaambia waandishi wa habari.



# Tembo Warriors kujichimbia Karatu

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania (TAFF), limesema Timu ya Taifa ya Tembo Warriors, leo Jumatatu itaelekea mjini Karatu, Arusha kuweka kambi ya muda mrefu kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika yatakayofanyika Aprili 14-29, mwaka huu, nchini Misri.

Awali, timu hiyo ilikuwa ikifanya mazoezi kwa wachezaji kwenda na kurudi nyumbani kwa kipindi cha mwezi mmoja katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Edward Salvatory.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa timu hiyo, Zaharan Mwenemti, alisema wameamua kwenda kuweka kambi hiyo Karatu kutokana na utulivu uliopo eneo hilo.

Alisema hizo zote ni jitihada za serikali chini ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT), ambalo limehakikisha wachezaji wanakaa kambini kwa muda mrefu ili kwenda kuliwakilisha vema taifa.

"Tunashukuru Baraza la Michezo la Taifa kwa kutuwezesha kupata kambi pamoja na kutugharamia gharama zote kuanzia kipindi tunafanya mazoezi ya kwenda na kurudi nyumbani hapa Dar es Salaam," alisema Mwenemti.

Meneja huyo alisema kambi hiyo itaambatana na michezo ya kirafiki nje na ndani ya nchi kwa lengo la kuimarisha miili ya wachezaji wao kabla ya kuelekea nchini Misri.

"Tunatarajia kucheza michezo ya kirafiki na timu ya watu wenye ulemavu Arusha tukiwa kambini kwa kupitia BMT tutapata mchezo wa kimataifa wa kirafiki kati ya Kenya, Uganda au Burundi na tutawahi mapema ili tupate nafasi ya kucheza katika kituo cha mashindano," aliongeza meneja huyo.

Alisema wanatarajia mashindano hayo yatakuwa magumu kutokana na kuongezeka kwa timu na kufikia 20, ambazo zote zitakuwa zikipambania kutinga hatua ya robo fainali, nusu, hatimaye fainali.

Aliweka wazi malengo yao kwanza ni ni kutetea nafasi iliyowawezesha kufuzu na kwenda kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia msimu uliopita ambapo waliishia hatua ya robo fainali.

# CHASAMBI AMTAJA BENCHIKHA SIRI KUANDIKA HISTORIA MECHI CAF

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba, Ladack Chasambi, amesema siri kubwa ya kuonyesha uwezo na kuingia katika historia ya wachezaji waliyoipeleka timu hiyo hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, ni kufuata maelekezo ya Kocha Abdelhak Benchikha, ambaye kila anapompa nafasi amekuwa akimwambia "nakuamini, kapambane".

Amesema Benchikha amekuwa akimsisitiza kujitoa kwa ajili ya timu jambo ambalo linamfanya kiwango chake kuwa bora na juzi kuwa miongoni mwa wachezaji waliofunga wakati wakishinda mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy katika mchezo wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Nyota huyo aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Mtibwa Sugar, juzi alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa kwa ngazi ya klabu akiingia katika kipindi cha pili na kufanikiwa kufunga bao lake la kwanza katika michuano hiyo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Chasambi alisema anafurahi kuwa miongoni mwa wachezaji walioingia katika historia kubwa ya kupeleka Simba robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa kwake ndio mara ya kwanza.

Alisema siri kubwa ya kuendelea kuonyesha uwezo mkubwa ni kufuata maelekezo ya benchi la ufundi ambapo Kocha Benchikha amekuwa akimwamini na kumtaka kufanya vizuri kila anapompa nafasi.

"Kocha amekuwa anaamini kila uwezo wa mchezaji ndani ya hii timu, amekuwa akinieleza juu ya uvimilivu, lakini kutaka kuniona najitoa, napambana kila anaponipa nafasi ya kucheza na kufuata yale ambayo amekuwa akielekeza," alisema Chasambi.

Aliongeza kuwa amekuwa akifanya hivyo kuanzia mechi ya FA dhidi ya TRA FC licha ya kwamba alifunga, lakini kikubwa kwake ni kucheza mechi kubwa na kufunga jambo ambalo limeingia katika historia ya maisha yake.

"Ni kweli kuna changamoto ya namba, lakini sina hofu juu ya ujio wangu Simba kwa sababu kocha anatoa nafasi na ninaimani nitaendelea kupambana na sitamwangusha kwa maamuzi yake," alisema Chasambi.



Kocha wa makipa wa Simba, Dani Cadena, wakipongezana na mshambuliaji wa timu hiyo, Pa Omar Jobe, baada ya mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana kumalizika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kushinda 6-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Hii ndiyo Simba ninayoitaka*

INATOKA UKURASA 24

ziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, na kupokelewa na Try Again, Mwenyekiti wa Klabu, Murtaza Mungungu na nahodha wa kikosi Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Kwa mantiki hiyo, wachezaji wa Simba na benchi la ufundi wameondoka na jumla ya Sh. milioni 530, kutokana na ushindi huo.

Katika hutua nyingine Rais Samia aipongeza Simba kwa kufanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku akisema ushindi wa mabao 6-0 walioupata si tu kwa ajili ya Simba pekee bali ni wa Watanzania wote.

"Hongereni sana Klabu ya Simba kwa kufanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Mafanikio yenu sio furaha na fahari kwa mashabiki na wanachama wa Simba, bali pia kwa Taifa na Watanzania wote," alisema Rais Samia.

Kocha Mkuu wa Jwaneng Galaxy, Morena Ramoreboli, pia ameipongeza Simba kwa mchezo mzuri na kutengeneza mashambulizi mengi na kushinda 6-0.

Alisema walipata wakati mgumu kuzuia Simba ambao walifanya mashambulizi kupitia wachezaji watano, akiwataja Kapombe (Shomari), Babacar Sarr, Said Ntibazonkiza, Chama, Fabrice Ngoma na Kibu Denis.

"Kipindi cha pili walifanya mabadiliko ambapo walimuingiza namba 34 (Ladeki Chasambi), walicheza kwa kasi na kufanikiwa kutufunga mabao matatu mengine, jumla kuwa mabao 6-0, nimebeba makosa na kupata funzo kupitia mchezo huu na kujipanga kwa muda mwingine," alisema Morena.

Hatua ya robo fainali Simba sasa inaweza kukutana na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Al Ahly ya Misri ama Petro de Luanda ya Angola.

# Gamondi amtaka yeyote

INATOKA UKURASA 24

kama ambavyo timu zote zilizomaliza nafasi ya pili zitafanya.

Yanga imemaliza Kundi D ikishika nafasi ya pili na pointi zake nane sawa na CR Belouizad ya Algeria, lakini ikasonga mbele kutokana na kanuni ya matokeo baina yake na timu iliyofunga pointi, maarufu kama 'head to head', ambapo pamoja na kupoteza ugenini kwa mabao 3-0, ilishinda nyumbani mabao 4-0, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa mabao 4-3.

Al Ahly ndiyo kinara wa kundi hilo, ikiwa na pointi 12, na kikanuni haziwezi kukutana na Yanga, huku Medeama ikishika mkia.

# Michezo

Jumatatu Machi 4, 2024

Nipashe




Mashabiki wamchoka Pochettino UKURASA 22

KITITA...




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, akikabidhi kitita cha Sh. milioni 30 kwa niaba ya Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwa viongozi wa Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', Murtaza Mungungu na nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala', kutokana na ushindi wa mabo 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Benchikha: Hii ndiyo Simba ninayoitaka

## Mdomoni kwa Mamelodi, Al Ahly, walamba milioni 530, Rais Samia...

**Na Saada Akida**

WAKATI mashabiki wa Simba wakiupokea kwa furaha kubwa ushindi wa kishindo kizito cha mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Abdelhak Benchikha, amesema "wachezaji wangu sasa wanaelekea kunipeleka kule kwenye Simba ninayoitaka".

**Katika mchezo huo wa kuhitimisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, unaifanya Simba kufuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi B, pamoja na Asec Mimosas ya Ivory Coast iliyoongoza kundi huku Wydad Casablanca ya Morocco na Jwaneng Galaxy zikiaga.**

Alisema anafuraha sana kwa wachezaji wake kuonyesha moyo wa kupambana na anaamini wataendelea kufanya vizuri katika mashindano hayo hatua ya robo fainali.

"Niwapongeze wachezaji, wamepambana sana na mashabiki kujitokeza kwa kusapoti timu yao, tulifanya maandalizi mazuri kwa kuzingatia mambo muhimu mbinu, ufundi, kisaikolojia kwa vijana wangu na kuwasisitiza katika kupambana.

"Wamefanya kile nilichowapa katika uwanja wa mazoezi kwa kushinda idadi kubwa ya mabao 6-0, kwangu tungeshinda bao 1-0 ingekuwa vizuri kwa kuwa tulihitaji kufuzu hatua nyingine," alisema Benchikha.

Kuhusu kiwango cha kiungo wake, Clatous Chama, kocha huyo alisema anaimani na uwezo wa nyota huyo ni mzuri hasa anapokuwa katika eneo la mpinzani.

"Ni mchezaji mzuri anakupa matokeo ukiangalia katika mchezo huu, ametoa pasi na amefunga bao, tumekosa nafasi nyingi tulizotengeneza ikiwamo mbili kutoka kwake," alisema kocha huyo.

Alisema baada ya mechi hiyo wanaenda kujipanga kwa ajili ya mechi zilizopo mbele yao ikiwamo za Ligi Kuu Tanzania kabla ya kufanya maandalizi ya kujiandaa na michezo ya hatua ya robo fainali.

Naye kiungo wa Simba, Chama alisema furaha yake si kutoa pasi wala kufunga bao bali ni kuona Simba inashinda kwa kuwapa furaha mashabiki wa timu hiyo.

Chama alisema haukuwa mchezo rahisi kwa kuwa walihitaji kupata ushindi ili kutinga hatua ya robo na wamefanikiwa hilo kwa kuwapa furaha mashabiki wanaoisapoti timu.

"Ni ushindi muhimu sana kwangu, timu ikishinda ni furaha sana kwa sababu tumewafanya mashabiki wetu wanaotusapoti kuwa na furaha, kwangu kufunga au kutoa pasi si jambo la kujivunia bali timu kushinda kwangu ndicho muhimu.

"Huu ni ushindi mkubwa na mzuri, hii ndio Simba inayohitaji jambo lake tumeingia hatua ya robo sasa tunajipanga kwa hatua nyingine, Simba hii weka mbali na watoto," alisema kiungo huyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa milioni 30 za 'bao la Mama' kutokana na ushindi wa mabao 6-0 walioupata dhidi ya Jwaneng Galaxy.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa zawadi hii, baada ya kuipata hii tunaenda kujipanga kwa ajili ya robo fainali na mipango yetu ya kuvuka zaidi, mbali na pesa hizo pia tumekabidhiwa Sh. milioni 100 kutoka kwa Rais wa Heshima wa Simba, Mohammed Dewji na klabu itatoa milioni 400 kama ahadi yao," alisema Try Again.

Kitita hicho cha Rais Samia kilikabidhiwa na Wa-

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi amtaka yeyote robo fainali CAF

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hana hofu na timu yoyote atakayokutana nayo kwenye hatua ya robo fainali na watakwenda kucheza kama wanavyocheza siku zote na klabu zingine.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo alikiri kuwa mechi za robo zote zitakuwa ngumu kutokana na kwamba timu zote zilizoingia ni nzuri na zenye uwezo mkubwa, lakini wao watacheza na yeyote kwa sababu imefika wakati ambao huwezi kuchagua wala kuomba kucheza na timu fulani.

Gamondi alisema hana hofu kwani ataendelea kucheza soka lake lile lile ambalo limekuwa likivutia watu wengi, iwe nyumbani au ugenini.

" Kama tumecheza na Al Ahly ya Misri, ni Mabingwa Watetezi Afrika, ni timu kubwa na yenye mafanikio makubwa nyumbani kwao, lakini hatukupaki basi, hivyo natumai kwa mechi zingine itakuwa hivyo," alisema Gamondi.

Naye Ofisa Habari wa timu hiyo, Ali Kamwe, alisema maandalizi ya kuelekea kwenye mechi mbili za robo fainali yameanza rasmi.

"Tumeanza maandalizi, nafikiri mechi za robo fainali zitapigwa mwishoni mwa mwezi huu, lakini kabla ya hapo tuna mechi za ligi kwanza ambazo zinatuweka vizuri kimazoezi na maandalizi.

"Michuano hii ni migumu na inahitaji pesa nyingi, kama klabu tumejiandaa vizuri na kila tunaposonga mbele tunajifunza kitu kipya na hizi mechi ni za kimahesabu sana, ukipiga hesabu zako vizuri, hasa kutumia vizuri mechi ya nyumbani, unaweza kusonga mbele," alisema Kamwe.

Yanga ambayo imemaliza kwenye nafasi ya pili, ina uwezekano mkubwa wa kukutana na Klabu za Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Asec Mimosas ya Ivory Coast ama Petro de Luanda ya Angola.

Itaanzia nyumbani na kwenda kumalizia mechi yake ugenini

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >